**DC**, Mkurugenzi Manispaa wafutwa kazi kisa machinga

UKURASA 2



**MAKALA MAALUM**

RC aingia na mkakati ajira 200,000 Simiyu

UKURASA 4


Wakulima walililia Bunge wamechoka na hadaa hizo

Hedhi inapoendelea kukwamisha wasichana mijini, vijijini kusoma

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

PROFESA MWESIGA BAREGU Ameondoka kabla ndoto kutimia

SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

Bajeti 2021/22 imwokoe mtoto na maafa uhaba sugu wa vyoo

UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatano Juni 16, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580613

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# Sakata maduka ya kubadili fedha laibuka bungeni

**MBUNGE** ahoji kama kuna watu serikalini wanataka kufanya biashara hiyo...

*Endelea Ukurasa wa 2*



Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo



# Samia ataja dawa tatizo ajira vijana

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**MSHTAKIWA AANGUA KILIO MAHAKAMANI**

MSHTAKIWA ambaye ni Kaimu Mkuu wa Idara ya Maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Mhandisi Rahel Buliba (38 ), ameangua kilio na...

**UKURASA WA 5**

**TAASISI YATAKA MABADILIKO SHERIA NDOA KULINDA MTOTO**

MKURUGENZI wa Sheria na Haki za Binadamu wa Taasisi ya Kujenga Jamii Jumuishi Tanzania (BISTO), Mussa Nzige, ameishauri serikali kurekebisha Sheria Ndoa ya Mwaka 1971 inayoruhusu...

**UKURASA WA 5**

**MAKALA AIBUA MKAKATI KUIFANYA DAR KUWA SAFI**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, ameandaa mkakati maalumu wenye miongozo 12 kwa ajili ya kuufanya mkoa kuwa safi. Amedokeza kuwa katika...


## KIWANDA B'MOYO KUPUNGUZA UHABA WA SUKARI

UKURASA 3


**MICHEZO** SIMBA, YANGA ZATANGULIA NUSU FAINALI YA VIJANA U-20 UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6

# Sakata maduka kubadili fedha laibuka bungeni

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

MBUNGE wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, ameibua tena sakata la suala la maduka ya kubadilishia fedha (bureau de change), akisisitiza serikali imepora fedha za wafanyabiashara wa maduka hayo.

Amesema jimboni kwake wafanyabiashara hao sasa wanateseka na kuhoji kama kuna watu serikalini wanataka kuifanya biashara hiyo.

Akichangia juzi bungeni jijini Dodoma mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22, mbunge huyo alisema kuwa jijini Arusha wamepata shida na kuteseka kutokana na vikosi ambavyo kila siku vimekuwa vikishindana kwenda huko.

"Vikosi hivi baadaye vikaja na mambo haya ya maduka makubwa ya kubadilishia fedha na watu wa maduka haya kuna mchezo wanaucheza ambao sijui watu wa serikali kuna ambao wanataka wafanye hii biashara, maana ukiangalia Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 mtaji wa mtu wa maduka haya ulikuwa Sh. milioni 40, wakaja mwaka 2017 wakaongeza Sh. milioni 100.

"Mwezi Mei mwaka 2018, wakaongeza hadi Sh. milioni 300, baadaye wakaona kila wakiongeza wale wanafanya biashara, baadaye wakaamua kuvamia na kwenda kuwapora.

"Wakapora fedha zao, wakapora magari yao, wakapora hati zao za nyumba, wakapora viwanja, wamebaki hoi, hili tatizo ni kubwa," alilalamika.

Februari 2018, Meneja wa Kitengo Kinachosimamia Fedha za Kigeni katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Eliyamringi Mandari, alisema BoT imeyafungia baadhi ya maduka.

Alibainisha kuwa Desemba maduka 63 yaliomba kusajiliwa upya ambayo leseni zao zilifutiwa na yaliyobaki kati ya 297, maombi yao yaliendelea na wengi waliyapeleka karibia mwishoni na walitoa mwezi mmoja kuyapitia na kutaka kama kuna nyongeza wazipeleke kabla ya Januari 31.

Alisema ilipofika mwezi huo mchakato huo ulifungwa lakini yapo maduka 65 maombi yao yalikuwa yanafanyiwa kazi.

"Hadi kufika mwisho wa tarehe hiyo maduka takribani 71 yalipewa leseni yakiwa na nyongeza ya matawi 40, hivyo jumla yakawa 111," alisema.

Aliongeza kuwa mpaka wakati huo wakizungumza, maduka 86 yalifutiwa leseni zao kwa kutotimiza masharti ikiwa ni pamoja na kutokuomba.

"Maduka 34 yaliomba kujitoa kwa sababu zao za kutotimiza hayo masharti, na kati ya maduka 86 mengi hayakuleta maombi na yaliyoleta yakashindwa kutimiza masharti, sharti kubwa ni namna ya kujieleza na kutoa viambatanisho sahihi vya fedha wanazotaka kuwekeza kwenye biashara hii zimepatikana kwenye vyanzo vipi," alisema.




Sehemu ya vijana waliohudhuria mkutano wa Rais Samia Suluhu Hassan katika Uwanja wa Nyamagana, jijini Mwanza jana. **PICHA: IKULU**

## DC, Mkurugenzi Manispaa watumbuliwa kisa machinga

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametangaza kutengua uteuzi wa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, SheilLa Lukuba.

Hatua hiyo ya Rais Samia inatokana na viongozi hao kuruhusu mgambo kuharibu mali za wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga na mamalishe katika manispaa hiyo.

Samia alitangaza hilo jana mkoani Mwanza alipokuwa akizungumza na vijana kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa katika Uwanja wa Nyamagana, mjini hapa.

Licha ya uamuzi huo, alimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kushughulikia suala hilo kwa kuwa tukio hilo lilikuwa la kusikitisha.

"Nimeona tukio lile la kudhalilisha wafanyabiashara wadogo wadogo pale Morogoro. Nimesikitika sana na natangaza Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wake hawana kazi," alisema.

Tangu aingie madarakani Machi 19, mwaka huu, hii ni mara ya nne kwa Rais Samia kutengua uteuzi wa viongozi mbalimbali serikalini.

Mara ya kwanza ilikuwa kwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, kwa kutangaza kumsimamisha kazi.

Mwingine aliyefuata ni Azza Hilal Hamad ambaye aliteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu lakini alitenguliwa kabla ya kuapishwa kuanza kutumikia nafasi hiyo. Kwa miaka kadhaa Hamad alikuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Mkoa wa Shinyanga.

Wiki iliyopita, Rais alitangaza kutengua uteuzi wa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Albert Chalamila, ikiwa siku 19 tu tangu alipohamia mkoani humo akitokea Mbeya.

# Rais Samia ataja dawa tatizo la ajira vijana

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amekiri kuwapo tatizo la uhaba wa ajira kwa vijana nchini na kubainisha mikakati ya kuukabili.

Akizungumza na vijana jijini Mwanza jana, Rais Samia alibainisha kuwa kwa sasa Tanzania ina vijana milioni 20.7 sawa na asilimia 40 ya Watanzania wote.

Rais aliweka wazi kuwa asilimia 11. 4 ya vijana wenye uwezo wa kufanya kazi nchini hawana ajira kutokana na uhaba wa fursa hizo.

Alisema ajira katika sekta za umma huendana na uwezo wa serikali kulipa mishahara ya watumishi wa umma na kwamba kwa sasa nafasi za ajira ndani ya serikali zimekuwa ngumu.

Rais Samia alisema ipo miradi ya kimkakati anayoamini itasaidia kutoa nafasi za ajira kwa vijana nchini.

Alisema miradi ya ujenzi wa daraja la JPM, bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, itawawezesha upatikanaji wa ajira nyingi kwa kundi hilo.

Rais alibainisha mkakati mwingine uliopo ni kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi ili itoe ajira kwa vijana.

Alisema mkakati mwingine ni kutoa fursa za kazi kwa serikali kujenga mazingira wezeshi kwa vijana kujiajiri wenyewe na kuajiri wenzao.

Alisema hilo limekwenda sambamba na kufuta tozo kwenye kilimo, mifugo na uvuvi na kwamba leseni za kibiashara sasa zinapatikana mitandaoni.

Rais Samia pia alisema serikali imeona fursa nyingine kwa kundi hilo katika sekta ya madini kwa kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo.

"Tumeanzisha hifadhi tano mpya na kupunguza tozo na kodi zilizokuwa kero kwenye utalii. Hii yote inatengeneza ajira nyingi kwa vijana," alisema.

Rais Samia pia alisema serikali inawezesha upatikanaji wa mikopo ya kielimu na biashara kwa vijana, akibainisha kuwa mwaka huu serikali imetenga Sh. bilioni 500 kwa ajili ya kugharimia mafunzo ya elimu katika vyuo vikuu na otahakikisha inawasaidia kibajeti kugharimia mafunzo katika vyuo mbalimbali vya ufundi.

Alisema anatambua bado kuna tatizo la upatikanaji wa mikopo kwa vijana na serikali itaanzisha benki kwa ajili ya kufanikisha azma hiyo.

Kwa mujibu wa Rais, benki hiyo itakuwa suluhisho kwa vijana kupata mitaji ya kuendesha biashara huku akiahidi kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya machinga na mamalishe.

Hata hivyo, aliwaonya machinga wanaopewa bidhaa kutoka maduka makubwa na kuviuza nje barabarani kwa kuwa hatua hiyo inaikosesha serikali mapato.

Rais Samia aliagiza kuundwa kwa baraza la vijana nchini ili kupata fursa ya kujadili mambo yanayowahusu. Baraza hilo, alisema pamoja na kupitiwa sera ya vijana, litasaidia kupaza sauti zao na kuona namna masuala yao yanavyoweza kushughulikiwa.

Kuhusu sekta ya sanaa, Rais Samia alisema kuanzia mwezi ujao, wasanii wataanza kulipwa mirabaha kwa kazi zao zinazopigwa katika redio, luninga na sehemu zingine.

Pia alisema serikali imeondoa kodi katika uingizaji wa nyasi bandia huku akiagiza Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutumia fursa hiyo kuboresha viwanja vya michezo.

Rais Samia aliwataka vijana kuacha kutumika kubeba wanasiasa na kuweka kando ajenda zao za maslahi ya vijana, akisisitiza 'waache mara moja'.

## HABARI KITAIFA



Mratibu wa Shirika la Maendeleo Vijijini (RDO), Fidelis Filipatali (wa pili kulia), akitoa maelezo ya mradi wa maji wa Mdabulo kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa, Happines Seneda (watatu kushoto) wakati akikagua miradi ya maji jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Kiwanda kupunguza uhaba wa sukari

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema uzalishaji katika kiwanda cha sukari cha Bagamoyo unatarajiwa kuanza Juni, mwakani.

Uzalishaji huo unatarajiwa kuanza na tani 30,000 hadi 35,000 na kitakapokamilika utafikia 100,000 kwa mwaka.

Kuanza kwa kiwanda hicho kutapunguza tatizo la upatikanaji wa bidhaa hiyo muhimu kwa matumizi ya nyumbani na viwandani ambalo limekuwa likiikumba nchi kila mwaka.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo juzi alipotembelea kukagua ujenzi wa kiwanda hicho na kujionea mashamba ya miwa na mabwawa ya maji kwa ajili ya umwagiliaji wa miwa.

Alisema moja ya vipaumbele vya serikali ni kuwekeza katika viwanda ambavyo vitazalisha bidhaa ambazo zinahitajika kwa kiasi kikubwa na moja ya bidhaa hizo ni sukari.

"Kwa sasa tuna mahitaji ya sukari ambayo ni tani 655,000 kwa mwaka lakini uzalishaji wa sasa kwa viwanda vyote ni tani 386,000. Mpaka Mei, mwaka huu, uzalishaji ulikuwa ni tani 256,000 ambayo ni asilimia 60 ya mahitaji yote na asilimia 40 inabidi tuagize kutoka nje ya nchi," alisema.

Waziri huyo alisema kwa sasa Tanzania kuna viwanda vya sukari takribani vitano ambavyo vilikuwa vya serikali wakapewa sekta binafsi ili kuviendeleza na kwamba kiwanda cha kuzalisha sukari cha Bagamoyo ni cha umiliki wa sekta binafsi kwa asilimia 100.

Naye Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Kampuni za Bakhresa ambaye ndiye mratibu wa mradi wa ujenzi wa kiwanda hicho, Hussein Sufian, alisema mradi huo unahusisha maeneo makubwa mawili kuendeleza shamba la kilimo cha miwa na ujenzi wa kiwanda.

Alisema ujenzi wa kiwanda umefikia asilimia 90 na kwamba tatizo lililopo ni ubovu wa miundombinu ya barabara kutoka Makurunge hadi kiwandani.

"Pia kuna tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji ya uhakika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji tunaona ni vyema kushirikiana na Wizara ya Maji ambao wana mpango wa kujenga bwawa kwa ajili ya utatuzi wa changamoto hiyo," alisema.

Sufian aliipongeza serikali kwa kushughulikia matatizo yaliyokuwa yakiwakabili kwa wakati na kuipongeza Serikali ya Wilaya ya Bagamoyo kwa juhudi inazofanya katika kuhakikisha kiwanda kinakamilika mapema kulingana muda uliopangwa.

"Kiwanda kwa awamu ya kwanza kinategemea kuajiri zaidi ya wafanyakazi 1,000 na baada ya awamu zote tatu kukamilika kiwanda kitaajiri zaidi ya wafanyakazi 4,000," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Zainab Kawawa, alisema serikali ipo katika mpango wa kumwongezea eneo mwekezaji huyo mzawa kati ya hekta 12,000 zilizobakia baada ya kupewa hekta 10,000 ili kumaliza tatizo la wavamizi wa ardhi.

# Mshtakiwa aangua kilio kortini

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

MSHTAKIWA ambaye ni Kaimu Mkuu wa Idara ya Maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Mhandisi Rahel Buliba (38 ), ameangua kilio na kumwaga machozi hadharani baada ya wakili wa Jamhuri kumbana kwa maswali katika Mahakama ya Wilaya ya Geita.

Tukio hilo lilitokea jana katika mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Samweli Maweda.

Mshtakiwa huyo alikuwa akitetewa na Wakili wa Kujitegemea, Penina Mashimba na kudai mahakamani kuwa mteja wake atajitetea peke yake kwa sababu hana shahidi lakini atakuwa na kielelezo kimoja.

Hakimu Maweda aliuliza upande wa Jamhuri kama wako tayari kwa ajili ya utetezi wa mshtakiwa na upande huo ukiongozwa na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Kelvin Murusuri, ulidai uko tayari.

Akiongozwa na wakili wake, alidai kuwa yeye ni Kaimu Mkuu wa Idara ya Maji katika Halmashauri ya Wilaya Geita na alisimamishwa kazi mwaka 2014 na kurudishwa mwaka 2019 baada ya kukata rufani katika ngazi za juu.

Alidai kuwa katika mikataba yote iliyofanyika yeye hakuhusika kutia saini bali ilitiwa saini na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Ali Kidwaka pamoja na mkandarasi mshauri anayejulikana kwa jina la COWI na Francis Nyenge.

Aidha, shahidi huyo alidai anaomba mahakama itupilie mbali mashtaka hayo kwa kuwa yeye hakuhusika na makosa hayo.

Baada ya mshtakiwa huyo kumaliza kutoa ushahidi wake hapo mahakamani, wakili Murusuri kwa kushirikiana na wakili wa serikali, Daniel Masambu walimwuliza mshtakiwa maswali kama ifuatavyo;

**Wakili:** Mkataba huu unautambua lakini sahihi yako haipo?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** Kazi unazopewa na Mkurugenzi lazima uandikiwe barua?

**Shahidi:** Kuna kazi zingine napewa barua lakini zingine sipewi barua.

**Wakili:** Kwenye mkataba huu ulikuwa unashirikishwa?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakaili:** Mkurugenzi huwa anapata taarifa kutoka kwako?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** Kuna kielelezo chochote ambacho umekileta hapa mahakamani kinachoonyesha kuwa wewe huwa unatoa taarifa kwa Mkurugenzi

**Shahidi:** Sijaleta kielelezo hapa mahakamani ila wakili wangu ataleta.

**Wakili:** Je, uliwahi kupata kielelezo cha kampuni hewa kutoka Uturuki ambacho umekileta hapa mahakamani?

**Shahidi:** Hapana sina pia sijatoa hapa mahakamani?

**Wakili:** Mwenye duka la spea za pikipiki ni nani wako?

**Shahidi:** Ni mzazi mwenzangu.

**Wakili:** Mbona ulidanganya mahakama kuwa haumfahamu Edes ambaye fedha milioni 75 ziliingia kwenye akaunti yake?

**Shahidi:** Mimi simfahamu Edes wala fedha hizo hazikuingia kwenye akaunti yangu.

**Wakili:** Una ugomvi gani na mzazi mwenzako Edes?

Baada ya kuulizwa hivyo, aliangua kilio na kudai ana ugomvi naye, lakini ni 'story' ndefu. Hatua hiyo ilisababisha hakimu kuahirisha kesi hiyo hadi Juni 23, mwaka huu.





Mkuu wa mkoa wa Simiyu, David Kafulila.

# RC aingia na mkakati ajira 200,000 Simiyu

## Aweka hadharani msimamo wake machinga barabarani

**"Endapo sisi tutaiona fursa hiyo na kuikimbilia, tutakuza na kutengeneza ajira nyingi sambamba na kukuza kipato cha mkoa," alisema.**

**Na Happy Severine, BARIADI**

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila ameahidi kutengeneza ajira mpya 200,000 kupitia shughuli mbalimbali zinazofanywa ndani ya mkoa huo.

Katika mazungumzo mahususi na Nipashe mkoani hapa, Kafulila anasema ajira ni moja ya vipaumbele vyake katika mkoa wenye umri wa miaka tisa sasa.

Anasema mkakati wake huo unalenga kufanyia kazi utekelezaji wa kilichoahidiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2020-2025.

Kafulila anakumbusha kuwa chama hicho kiliahidi kutengeneza ajira milioni nane katika kipindi hicho cha miaka mitano.

Anasema katika kutekeleza ahadi hiyo, yeye atahakikisha anatengeneza ajira 200,000, sawa na asilimia 2.5.

Kafulila anasema kwa kutambua umuhimu wa suala hilo, kitu cha kwanza atakachokifanya ndani ya mkoa huo ni kuhakikisha anatengeneza ajira hizo 200,000 kupitia shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi kwa kushirikiana na viongozi wenzake.

Kafulila ambaye aliwa kuwa mbunge kupitia chama cha NCCR-Mageuzi kati ya mwaka 2010 hadi 2015 kwenye Jimbo la Kigoma Kusini, anasema atatengeneza nafasi hizo ili vijana na makundi mbalimbali yaweze kuajiriwa na kujiajiri.

Mkuu wa mkoa huyo anasema atakuwa anashirikiana na viongozi wenzake, wataalamu na wafanyabiashara wa ngazi zote mkoani humu kufikia lengo hilo.

Kafulila pia anawataka maofisa biashara wa wilaya zote kuhakikisha wanatafuta mbinu rahisi za kuwasaidia wafanyabiashara wadogo kupata vitambulisho vya ujasiriamali kutokana na ugumu uliopo katika upatikanaji wake.

Anasema kwa sasa utaratibu wa upatikanaji wa vitambulisho hivyo ni kwa mfanyabiashara mwenyewe kujaza fomu na kujipiga picha kwa njia ya mtandao, jambo ambalo linasababisha washindwe kufanya kazi hiyo kwa kuwa baadhi yao hawana utaalamu huo.

Anawataka maofisa hao kuangalia namna rahisi kama ambavyo watu wa benki wanawafuata katika kuwafungulia wateja wao kadi za papo kwa papo ili hata wale wa vijijini wavipate kwa urahisi.

Kuhusu tatizo la machinga kupanga bidhaa barabarani na kuhatarisha usalama wa raia, Kafulila anasema anapanga muda wa kukutana nao kwa ajili ya mazungumzo.

Anabainisha kuwa katika mazungumzo hayo, watajua ni eneo gani sahihi ambalo litatumia kwa ajili ya biashara zao.

### FURSA ZA UWEKEZAJI

Baadhi ya wananchi mkoani Simiyu wanataja fursa za uwekezaji zinazopatikana katika mkoa wao kuwa ni pamoja na kilimo cha viazi lishe na alizeti ambacho wanaamini kitasaidia kuongeza ajira na kukuza vipato vyao.

Wanasema kuna fursa za ajira kupitia mazao hayo kwa kuwa mkoani mwao kuna viwanda vitumiavyo malighafi hizo.

Anitha Alphone, mkazi wa Mji wa Bariadi, anasema wananchi wanatakiwa kuziona fursa hizo kama njia mojawapo ya kujikwamua kiuchumi kwa kuwa mkoa huo una viwanda vya mafuta ya alizeti na kiwanda cha viazi lishe lakini upatikanaji wa malighafi zake ni wa shida.

"Endapo sisi tutaiona fursa hiyo na kuikimbilia, tutakuza na kutengeneza ajira nyingi sambamba na kukuza kipato cha mkoa," alisema.

Costantine Mathias, mkazi wa Nyangokolwa, anasema wengi bado hawajaiona fursa hiyo, hivyo elimu na mikakati zaidi inatakiwa ili kukuza uzalishaji huo.

### KUHUSU SIMIYU

Mkoa wa Simiyu ulianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 72 la Machi 2, 2012. Unapatikana kaskazini mwa Tanzania, kusini mashariki mwa Ziwa Victoria.

Kwa upande wa Kaskazini, Mkoa wa Simiyu unapakana na Mkoa wa Mara; upande wa mashariki mikoa ya Arusha, Singida na Manyara; kusini mikoa wa Shinyanga na Tabora na upande wa magharibi Mkoa wa Mwanza.

Kwa mujibu wa tovuti rasmi ya Mkoa wa Simiyu, mkoa huo una eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 23,807.7.

Eneo linalofaa kwa shughuli za kilimo na ufugaji ni kilomita za mraba 11,479.1, kilomita za mraba 11,723.6 ni eneo la Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Mapori ya Akiba ya Maswa, Kijereshi na Mwiba; na Hifadhi za Jumuiya za Wanyama Pori ya Makao (WMA) iliyoko katika Wilaya ya Meatu na kilometa za mraba 605 ni eneo la maji ya Ziwa Victoria.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Mkoa wa Simiyu ulikuwa na jumla ya wakazi 1,584,157; wanaume wakiwa 759,891 na wanawake 824,266.

Mkoa huo una ongezeko la watu wa wastani wa asilimia 1.8 kwa mwaka, ukipishana kidogo na wastani wa kitaifa wa asilimia 2.7.

Hali ya mvua kwa mwaka ni wastani wa kati ya 600mm hadi 900mm. Katika baadhi ya maeneo (Meatu) kiasi cha mvua ni 400mm. Hali ya joto ni kati ya 18°C hadi 31°C.

Kwa ujumla, kuna misimu miwili ya mvua; msimu wa mvua za vuli kati ya Oktoba hadi Desemba na ule wa masika kati ya miezi ya Februari na Mei kila mwaka.

Kiutawala, Mkoa wa Simiyu unaundwa na wilaya tano zenye majimbo saba ya uchaguzi (Itilima, Bariadi, Maswa Mashariki, Maswa Magharibi, Busega, Kisesa na Meatu); na halmashauri sita.

Vilevile, mkoa huo una tarafa 16, kata 130, vijiji 471 na mitaa 92. Mkoa huo una shule za sekondari 152 na za msingi 524.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kushoto), akikabidhi meza 12 na viti viwili, kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Ngokolo, Malale Masali, kwa ajili ya walimu wa shule hiyo, Manispaa ya Shinyanga, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Taasisi yataka mabadiliko sheria ndoa kulinda mtoto

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI wa Sheria na Haki za Binadamu wa Taasisi ya Kujenga Jamii Jumuishi Tanzania (BISTO), Mussa Nzige, ameishauri serikali kurekebisha Sheria Ndoa ya Mwaka 1971 inayoruhusu mtoto chini ya miaka 18 kuolewa kwa ridhaa ya mzazi kama ilivyoamuliwa na Mahakama ya Rufani.

Nzige aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo hufanyika Juni 16 kila mwaka.

Alisema kwenye kesi ya msingi namba 204 ya mwaka 2019 iliyoamuliwa na Mahakama ya Rufani kuwa kifungu cha 13 na 17 cha sheria hiyo kinapingana na Katiba ya Tanzania ya 1977 kwa kuweka umri tofauti wa kuoa au kuolewa kati ya mtoto wa kike na wa kiume.

Nzige alisema serikali inatakiwa kubadilisha sheria hiyo ambayo ina ubaguzi kwa watoto wa kike na wa kiume ndani ya mwaka mmoja mpaka sasa umekwisha na hakuna jitihada zozote zilizochukuliwa katika kutekeleza maamuzi ya mahakama.

Aidha, alisema Siku ya Mtoto wa Afrika, mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuwa yakishirikiana na serikali katika kutoa elimu na kufanya ushawishi wa sera mbalimbali ili kuleta ustawi wa maendeleo ya taifa.

"Leo hii kituo cha kupinga ukatili wa kijinsia (CAG-BV) kwa kushirikiana na Taasisi ya Bisto kwa pamoja katika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika mwaka huu, na kuunga mkono uamuzi wa kitaifa na kimataifa imeona iangalie haki za watoto na hasa wale watoto wenye ulemavu hapa nchini," alisema.

Nzige alisema katika ajenda ya mwaka 2040 kundi la watoto wenye ulemavu bado limekuwa na mafanikio na changamoto zinazowafanya wasifurahie utoto wao kama watoto wengine.

Alisema kundi ambalo limekuwa likisahaulika bila kutajwa kwa upekee wake kama kundi maalum, hivyo jamii inatakiwa kuelewa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ambayo ni msingi wa kutekeleza na kumlinda mtoto wanapotekeleza ajenda ya 2040. Alisema watoto wenye ulemavu baadhi yao wamegeuzwa kitegauchumi na kunyimwa haki zao za msingi jambo ambalo halikubaliki.

"Kama una nguvu kwa nini usiende kufanya kazi na kumsaidia huyo mtoto badala ya kumgeuza kitega uchumi na kuzunguka naye kutwa ili ujipatie hela," alisema.

Aidha, alisema Tanzania ilipitisha sera ya maendeleo ya mtoto ya mwaka 2009 inayoelezea haki za mtoto. Mbali na nchi hizo imesaini mikataba mengine ya kimataifa kumlinda mtoto kama vile sheria ya utumikisha wa watoto katika vita, kwenye kazi na masuala ya kingono.

# Makala aibua mkakati kuifanya Dar kuwa safi

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, ameandaa mkakati maalumu wenye miongozo 12 kwa ajili ya kuufanya mkoa kuwa safi. Amedokeza kuwa katika miongozo hiyo, amesema ameanza na mitatu.

Makala aliyasema hayo jana wakati wa kikao kazi alichokifanya na viongozi wa kiserikali katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke huku akibainisha kwamba hali ya usafi katika mkoa si nzuri na haridhishwi nayo.

Alisema mkoa huo ni lango la kibiashara na ndio uso wa nchi kwa kuwa kuna vitu mbalimbali vikiwamo bandari, uwanja wa ndege wa kimataifa ambao wageni wengi wanaoingia nchini hupitia hapo lakini mazingira ya usafi hayaridhishi na hayapaswi kuachwa yalivyo.

"Suala hili nalisemea kwa nguvu zangu zote bila uoga. Mimi mkuu wenu wa mkoa sijaridhishwa hata kidogo na hali ya usafi katika mkoa wa Dar es Salaam. Juzi nilienda 'airport' (uwanja wa ndege) kumpokea Rais wa Botswana yaani nilitamani magari yao yangekuwa hayaoni nje.

"Kuanzia uwanja wa ndege unakuja mpaka Mnazi Mmoja ni vibanda, takataka, Moshi, mtu anapika na mkaa na gesi pembezoni mwa barabara. Ni aibu kosa si wale wanaofanya ila ni sisi tulisahau wajibu wetu wa kuwaweka vizuri. Vibanda kila mahali hakuna mahali utapita vizuri sehemu za watu kupita kote ni vibanda," alisema.

Makala aliongeza kuwa kutokana na hali hiyo, ililmlazimu kuandaa mwongozo utakaosaidia kuuweka mkoa katika hali ya usafi.

Alibainisha kuwa kuna watu wanafanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi na wamejenga vibanda juu ya mifereji jambo ambalo litakwamisha jitihada za kusafisha mifereji hiyo, hivyo watapangwa sehemu sahihi ili kuruhusu usafi uendelee kufanyika.

"Mtu anajua kabisa kuwa hapa nilipo si mahali pazuri. Hatuwezi kuwa na sehemu ambayo mtu anaweza kupika popote, tutakwambia hapa hapafai kupika kapikie pale, hapa ulipo unawaziba watu watembea kwa miguu, hapa ulipo unatukwamisha wazibua mitaro kwa hiyo kuna haja ya kuwapanga vizuri," alisema.

Mwongozo wa pili, alisema ni usimamizi wa usafi kwamba kuna makandarasi wanapewa kazi lakini wengine hawana uwezo, hivyo waambiwe inatosha na wapewe watu wenye uwezo wa kuendesha uzoaji wa taka kwa weledi.

Alisema suala hilo atalisimamia kwa kuwa anajua gharama yake kwa sababu linagusa maslahi ya watu na kwamba kwa kuwa anasimamia haki, ataendelea kutimiza wajibu wake katika kuuweka mkoa huo kuwa safi. Aliwataka viongozi wengine kuwa wakali na kuhakikisha kampuni zinazopewa tenda zinakuwa na uwezo.

"Uongozi ni kutambua tatizo na kulirekebisha. Ukiwa unatambua tatizo na wewe huonyeshi nia ya kutatua tatizo wewe pia ni tatizo. Mimi lawama hizo sizitaki, nachukua watu wangu wa uongozi, niwashawishi waheshimiwa madiwani kwamba lazima tuiweke Dar es Salaam safi. Nendeni nchi yoyote utaratibu huo upo hapa fanya hapa usifanye.

"Dar es Salaam sasa imekuwa kama tumeruhusu kila mtu afanye analotaka. Hakuna anayejali yaani kungekuwa na barabara ambayo magari hayapiti mara kwa mara naamini mtu angeweza kupika katikati ya barabara. Lazima tujenge heshima ya mji wetu ni mji mkubwa wa kibiashara na unapokea watu mbalimbali. Ni lazima tuuweke katika madhari mazuri ya usafi," alisema.

Mwongozo wa tatu alisema ni elimu ya usafi kwa sababu watu hawajahamasishwa, hawajaelezwa kwamba usafi unaanza na familia nyumbani na mtaani na kutokuwa na uelewa wa mahali sahihi pa kutupa taka.


**TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC**

**MARUDIO**

**Mwenyekiti na Wanahisa,**

**Yah: Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa**

Taarifa inatolewa kwamba **Mkutano Mkuu wa Saba wa Wanahisa wa Tandahimba Community Bank** utafanyika siku ya **Jumamosi tarehe 19 Juni, 2021,** katika **Maghala ya Chama cha Ushirika TANECU,** Tandahimba kuanzia saa tatu kamili **(Saa 3.00)** asubuhi kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuridhia Dondoo.**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliopita.**
4. **Kujadili yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita.**
5. **Kujadili na kupokea Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2020.**
   - 5.1 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.
   - 5.2 Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2020.
6. **Taarifa kuhusu Mtaji wa Benki.**
7. **Kuidhinisha Uteuzi wa Mkurugenzi wa Bodi.**
8. **Kuidhinisha Ada ya Wakurugenzi.**
9. **Kuteua Wakaguzi wa Hesabu.**
10. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
11. **Kupanga mahali na tarehe ya Mkutano ujao.**
12. **Kufunga Mkutano.**

**Maelezo:**

1. *Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 18/06/2021 na litafunguliwa tena tarehe 21/06/2021.*
2. *Makabrasha ya Mkutano yatapatikana katika Makao Makuu ya Benki kuanzia tarehe 07/06/2021 na kwenye Ukumbi wa Mkutano tarehe 19/06/2021.*
3. *Wanahisa wana haki ya kutuma wawakilishi kwa kuwapa hati ya hisa na fomu ya uwakilishi iliyojazwa kikamilifu.*
4. *Wanahisa watakao hudhuria Mkutano watajigharamia usafiri na malazi.*

**Kwa mawasiliano tafadhali tumia anuani ifuatayo:**
**Katibu wa Benki,**
**Tandahimba Community Bank Plc,**
**S. L. P. 06, Tandahimba. MTWARA.**

**KWA IDHINI YA BODI**

**J. B. Rugambo**
**KATIBU**
**20 Mei, 2021**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jitihada kumlinda mtoto ziimarishwe

LEO ni Siku ya Mtoto wa Afrika, mahususi kwa ajili ya kukumbuka mauaji waliyofanyiwa wanafunzi wa Soweto, Afrika Kusini Juni 16, mwaka 1976.

Siku hii wadau mbalimbali wa maendeleo ya mtoto huitumia kueleza vikwazo dhidi ya mtoto wa Afrika, hasa kwa mazingira ya Tanzania.

Licha ya jitihada mbalimbali za kumwezesha mtoto kufikia ndoto zake, lakini bado kuna vikwazo kadhaa ambavyo vimesababisha kushindwa kufikia ndoto zake.

Kwa sasa matukio la ulawiti watoto wa kiume yanaongezeka kiasi cha kuwaathiri kisaikolojia, kimasomo na maisha yao ya baadaye, na mengi ni yanayotendwa na ndugu wa karibu, wanafunzi au wanajamii.

Pia matukio ya ubakaji ni kikwazo kikubwa kwa kuwa wapo walioshindwa kuendelea na masomo yao, wamepata magonjwa kama ya Ukimwi au mimba na kuwa mwisho wakufikia ndoto zao. Baadhi kuna ukatili wa ukeketaji kwa kisingizio cha kutimiza matakwa ya mila za jamii fulani, huku ndoa za utotoni zikishika kasi katika baadhi ya maeneo.

Kikwazo kingine ni utumikishwaji wa watoto kwenye kazi ngumu tofauti na umri wao, jambo ambalo halipaswi kuwa hivyo bali wanatakiwa wawe shuleni badala ya kuwa wafanyakazi wa ndani au kwenye migodi.

Baadhi ya maeneo mtoto wa kike haruhusiwi kuendelea na masomo na wazazi huingilia katika kumtaka afanye vibaya darasani, ili asiendelee na masomo bali aolewe, jambo ambalo siyo sahihi kwa watoto.

Aidha, kutokana na kuongezeka kwa kampeni za hamasa ya kumwinua au kumnusuru mtoto wa kike, wa kiume wamesahaulika kiasi cha kuendelea kushamiri kwa matukio yanayowasababishia madhara.

Tunatambua jitihada za serikali katika kumlinda mtoto wa Kitanzania kwa kuhakikisha kuna sera na sheria za kumlinda mtoto dhidi ya matukio yoyote ambayo yana adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela iwapo utapatikana na hatia ya kumpa mimba au kumkeketa mtoto.

Licha ya jitihada hizo, bado kuna changamoto kwenye kifungu cha13 na 17 cha Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, ambayo inapingana na Katiba ya nchi ya 1977, kwa kuweka umri tofauti wa kuoa au kuolewa kati ya mtoto wa kike na wa kiume.

Sheria hiyo inayoruhusu mtoto chini ya miaka 18 kuolewa kwa ridhaa ya mzazi, hatua ambayo imeathiri watoto wengi, kwa kuwa kwa umri huo bado ni mtoto na anatahili kuwa chini ya wazazi. Baadhi ya wadau wamepinga kifungu hicho mahakamani, ambayo iliielekeza serikali kufanya mabadiliko ya vifungu hivyo.

Tunaamini kuwa vikwazo vyote vinapaswa kushughulikiwa kwa pamoja, kwa maana ya wadau na serikali ili kuendelea kumsaidia na kumwezesha mtoto kutimiza ndoto zake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# 'Vilio' awamu ya tano vinapoibua katiba mpya

Na Miki Taseni

MALALAMIKO dhidi ya awamu ya tano, yanatajwa kuwa yanarudisha fikra za wanaharakati wa nje na ndani kutamani kuwapo na katiba mpya.

Ni kwa sababu hisia tofauti zinaendelea kujitokeza kuhusu nini cha kufanya kurekebisha upungufu ulioonekana miaka kadhaa iliyopita kuminya uhuru wa kujieleza na haki ya kutoa maoni.

Awamu ya tano ilibana uhuru wa vyombo vya habari na shughuli za kisiasa zilizuiliwa kwa maelezo kuwa ni wakati wa kujenga nchi siyo muda wa kazi za kisiasa.

Kufuatia hali hiyo wako wanaosema kuwa kinachohitajika ni semina elekezi kwa viongozi kuhusu matumizi ya mamlaka na baadhi wanaoendeleza harakati kwa miaka mingi wanapendekeza ujio wa katiba mpya.

Semina elekezi zilisaidia kiasi kuleta maelewano kati ya viongozi, kuboresha utaratibu wa kupeana taarifa au kueleza matatizo wanayopata watendaji, lakini matatizo ya msingi yalibaki katika uongozi kwani hulka zilibakia kama zilivyokuwa.

Kwa maana hiyo hisia kuwa 'kutofundwa' katika semina elekezi au makuzi kwa jumla ya uongozi katika chama na serikali ni chanzo cha matatizo ni kutokuona uhalisi wa udhaifu wa mifumo, kuwa hakuna ushindani wa kisiasa unaolenga sera, ila utii kwa viongozi.

Ina maana kuwa mwelekeo wa awamu ya tano wa kunyamazisha makundi yote ya kisiasa ila katika kutenda shughuli walizonazo kiserikali ilisaidia kupunguza hamasa nchini, kujiamini kwa viongozi na mfumo kubebeshwa mzigo wa kuongea na kila mmoja na kuelewana.

Kunyamazishwa huku kumesaidia mabadiliko na mshikamano unaoonekana sasa.

Ni wazi kuwa wana-CCM na wadau wengine wa siasa wanahitaji kutafakari jinsi ya kutumia kipindi hiki cha mpito ambako demokrasia pana bado haijarudi kikamilifu, kuweka mazingira ya kiuchumi ambayo hata demokrasia hiyo ikirudi hayatavuruga umoja na mshikamano.

Bila uchumi shindani na ambako kuna ustawi, haitawezekana kuendeleza umoja wa nchi ndani ya demokrasia pana, kwani walioko nje ya madaraka wanataka waingie kwa nguvu zote, waanze 'kula'. Hawana haja ya kuonyesha nini kinahitaji kurekebishwa na kwa njia gani, ila kusisitiza kuwa serikali si halali.

Mifano ya kujifunza ni mingi, kuwa nchi zenye uchumi imara na shindani pia zinamudu ushindani wa kidemokrasia na kinyume chake kwa hizo zilizobaki. Yako maeneo mengine ambako utamaduni ni nyenzo ya utawala wa kidemokrasia kama Uingereza, ila kwa Afrika ni muhimu kukumbuka kuwa hakuna vianzio vya kutosha vya umoja wa kitaifa kwani jamii za jadi ndizo zimeshika sehemu kubwa ya nchi, hivyo mshikamano wa kisiasa huanzia katika jadi na kujipanua kutaka ushike mamlaka ya nchi.

Makundi ya haki za binadamu hayajafanya kazi ya kutosha ya kutafiti nini kinachowezesha demokrasia isimame bila kuteteresha umoja wa nchi na uwajibikaji serikalini.

Ni kweli wanaendelea kujitahidi pale nchi inapoonyesha dhamira ya kuendeleza utawala bora, lakini mara nyingine inabidi nchi ifanye kazi ya mabadiliko halafu wananchi watazamie kuwa baadaye wataelewa.

Tanzania hivi sasa inaelewana na mataifa mengi yaliyoendelea kuliko katika awamu ya tano, ila ikumbukwe kuwa Tanzania yenye utulivu na mipango mikubwa ya maendeleo ambayo inatekelezwa kwa ari na uadilifu isingekuwapo bila hatua za awamu ya tano. Hata hivyo zilifanyika bila kuwapo na 'semina elekezi.'

Hata hivyo kazi ngumu zaidi ya awamu ya sita siyo tu kukamilisha miradi mikubwa iliyopo na maeneo kadhaa ya ustawi wa jamii na pia kubuni mbinu za kujenga uchumi shindani unaoweza kustahimili vishindo vya demokrasia pana inapojikita kisawasawa.

HABARI KITAIFA

# Mbunge asifu kadi nyekundu ya Samia

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Tabora Mjini (CCM), Emmanuel Mwakasaka, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuchukua hatua kwa kiongozi aliyetumia ulimi wake vibaya.

Mwakasaka ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, alitoa pongezi hizo jana bungeni wakati akichangia mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Alimpongeza Rais Samia kwa kuonyesha kadi nyekundu kwa kiongozi huyo wa serikali na kueleza kuwa hiyo ni dalili kwamba anafanya kazi nzuri na inaleta heshima kwa nchi.

"Ninampongeza Rais Samia kwa namna alivyoanza hata humu ndani kumetulia, tunampongeza kwa uteuzi mbalimbali na tuliambiwa ana kadi ya njano na nyekundu na tumeona moja imetumika juzi juzi.

"Na kwenye mpira kuna kadi unapewa moja kwa moja nyekundu bila kuonywa, na sisi Kamati ya Maadili moja ya maadili ya viongozi ni pamoja na kutumia lugha ya staha.

"Ninampongeza sana Rais kwa kumwonyesha kadi nyekundu kiongozi mmoja wa serikali ambaye ametumia ulimi wake vibaya," alisema.

Mbunge huyo alisema moja ya maadili ya kiongozi wa serikali ni kutumia ulimi vizuri kwa kuzungumza lugha ya staha na kwamba kiongozi huyo aliweka komedi, akazidisha kwa kutumia lugha ambayo siyo ya staha, hivyo ameonyeshwa kadi nyekundu moja kwa moja.

## Raia wa Congo watupwa jela kuishi bila vibali

**Na Kulwa Mzee**

RAIA wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) Didi Hamed, anayedai alikimbia mlipuko wa volcano nchini humo na kuingia Tanzania pamoja na wenzake wawili waliokimbia machafuko, wamekwenda jela mwaka mmoja baada ya kukutwa na hatia ya kuishi nchini bila kibali.

Washtakiwa hao walihukumiwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, baada ya kukiri makosa yao.

Waliokwenda jela ni Didi (35), Fida Joseph (49) na Fred Nsengo (49). Baada ya mahakama kuwakuta na hatia, waliiomba iwapunguzie adhabu.

Mshtakiwa Didi alidai DRC ulitokea mlipuko wa volcano na ndugu zake wamekufa hivyo akaamua kukimbilia Tanzania na kwamba ana wadogo zake wawili wanamtegemea, hivyo akaomba asipewe adhabu kali.

Nsengo alidai anaomba asipewe adhabu kali kwa kuwa yeye anatokea Ben eneo la Congo kwenye machafuko, hivyo hata kama atarudi hana mahali pa kufikia.

Fida Joseph anadai alikuwa msusi huku wenzake walidai kwamba walikutwa bado hawajapata kazi za kuajiriwa.

Washtakiwa walikiri makosa na mahakama iliwatia hatiani na kuwapa adhabu ya kila mmoja alipe faini ya Sh 500,000 au jela mwaka mmoja na wakimaliza adhabu hiyo wahalalishe ukazi wao au warudi nchini kwao.

Awali, akisoma maelezo ya kosa, Wakili wa Serikali kutoka Idara ya Uhamiaji, Shija Sita, alidai washtakiwa hao walitenda kosa hilo Juni 14, mwaka huu.

Wanadaiwa katika tarehe hiyo walikutwa Sinza wakiishi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kibali.

Washtakiwa hao walipelekwa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Dar es Salaam na kuchukuliwa maelezo kisha kufikishwa mahakamani.

Washtakiwa wote wameshindwa kulipa faini hivyo, hivyo kwenda gerezani kutumikia kifungo.




Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi (kushoto) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng'wanakilala wakizindua mfumo wa HAKI YANGU App, jijini Dar es Salaam jana, uliobuniwa na LSF kwa ajili ya kumsaidia mwananchi kupata huduma ya msaada wa kisheria popote alipo kupitia simu yake. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Killango apiga magoti bungeni

**Na Romana Mallya,** DODOMA

MBUNGE wa Same Mashariki, Anne Killango Malecela, jana alichangia bungeni mjadala wa mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha akiwa amepiga magoti.

Anne alisema alilazimika kuchangia kwa mtindo huo kwa kuwa alikuwa anawasilisha taarifa ya wananchi ya kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wa serikali yake kuhusu bajeti ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

Akizungumza bungeni jijini Dodoma, Anne aliwataka wabunge wenzake badala ya kwenda Dubai, waende majimboni mwao kusimamia fedha zilizotengwa kwa ajili ya TARURA.

"Tangu tumeanza Bunge kila mbunge anayesimama anazungumzia TARURA, tumezungumza TARURA miaka mingi iongezwe fedha, sasa tabia ya wanawake ipo hivi hata kama ana homa amelala kitandani mtoto akilia ananyanyuka anamwangalia kwa nini analia, wabunge mmelia sana mama ana kazi nyingi lakini amenyanyuka," alisifu.

Mbunge huyo alisema wabunge wamelalamika kuhusu barabara hizo za vijijini na kuwaeleza kuwa safari za Dubai 'hapana', wakasimamie fedha hizo kwenye majimbo yao.

"Ninatoa onyo kwa mameneja wa TARURA, hizi Sh. milioni 500 zisipotee, wabunge safari za Dubai, sijui India hapana, tuende majimboni tukazisimamie hizi Sh. milioni 500," alisema.

Kuhusu ulipaji wa kodi, mbunge huyo aliitaka serikali isilichukulie suala hilo kiutani kwa kuwa wanaposafiri kwenda nchi zingine wajifunze.

"Nilikwenda China, kabla hawajafunga mipaka, nikienda ninakaa siku tano na ni lazima nizunguke na mkalimani, nikiwa huko nilimwambia mkalimani nichukulie muhindi, nilipopewa nikamwona mzee anayeuza ameshika simu anaandika, nikamuuliza mkalimani akaniambia analipa kodi.

"Kuna fedha nyingi tunaziacha, tafuteni njia ya kuzikusanya, wapeni elimu wananchi walipe kodi bila shuruti," alisema.

Mbunge huyo alimshauri waziri kuhusu ulipaji kodi ya majengo, akimtaka wakauangalie vizuri kwa sababu mtaani kuna mkanganyiko.

"Mkaliangalie vizuri hili jambo, mkaliweke vizuri kwa wananchi wawe na raha, hatupendi bajeti hii ya mwanzo ya Rais iwe na maneno maneno huko nje," alisema.

# Corona yahusishwa kupanda bei mafuta

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

BARAZA la Kilimo Tanzania (ACT), limeishauri serikali kuandaa mikakati ya kuzalisha mafuta ya kula kuwapo kwa uhaba wa bidhaa hiyo kutokana na nchi zinazozalisha mafuta kukabiliwa na janga la corona, hiyo kusababisha kupanda kwa bei.

Mkurugenzi Mtendaji wa ACT, Timoth Mmbaga, alisema kutokana na kuwapo kwa janga la corona, kumesababisha nchi hizo kuzuia mafuta ziliyokuwa zikizalisha kwa hofu ya kukosa malighafi, hivyo kufanya bidhaa hiyo kupanda kwa nchi mbalimbali, ikiwamo Tanzania.

Mmbaga aisema hayo katika kikao cha wadau wa uzalishaji wa alizeti kujadili mnyororo mzima wa zao hilo uliofanyika mjini haba jana.

Alisema uzalishaji wa mafuta ya kula nchini ni asilimia 40 na asilimia 60 huagizwa nje ya nchi, hivyo lengo la kukutana wadau hao ni kupanga mikakati ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ufikie asilimia 100, hivyo kujitosheleza kwa bidhaa hapa nchini.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, hali hiyo imesababisha uzalishaji wa mafuta kidunia kuwa mdogo na bei kupanda badala ya kushuka pamoja na serikali kuagiza mafuta nje ya nchi.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wasindika Mbegu za mafuta (TUSUPA), Ringo Iringa, alisema mahitaji ya mafuta nchini ni tani milioni 1.7 kwa mwaka wakati uzalishaji wake ni tani 352,908.

Mwenyekiti huyo alisema sababu mojawapo inayochangia uzalishaji mdogo ni pamoja na upatikanaji wa mbegu wakati mahitaji ni tani 5000 za alizeti kwa mwaka huku uzalishaji ukiwa tani 539 kiwango ambacho ni kidogo sana.

Alisema mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni tani 570,000 wakati uzalishaji wa viwanda vya ndani uwezo wake ukiwa ni 205,000 na hivyo kulazimika kuagiza tano 395 nje ya nchi.

Licha ya Tanzania kuwa ya kwanza katika nchi za Afrika kuwa na viwanda vingi vya kuchakata mafuta ya alizeti, alisema uzalishaji wa mafuta ni mdogo, hivyo kulazimika kuagiza mafuta nje ya nchi.

Alisema Tanzania ina viwanda 773 vya kuchakata mafuta ya kula ambavyo ni vikubwa na vidogo huku Afrika Kusini ikiwa na viwanda 12 vikubwa lakini ndio nchi inayoongozwa kwa kuzalisha mafuta ya kula katika Afrika.

Pamoja na kuwapo kwa changamoto hizo, aliwataka wakulima na wazalishaji wa alizeti kutopandisha bei ya mafuta na badala yake waiombe serikali kusaidia kupunguza changamoto zinazowakabili wakulima.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo kutoka Hanang mkoani Manyara, Geoffrey Jacob, alisema tatizo kubwa ni upatikanaji wa mbegu za alizeti na zile ambazo zinapatikana bado zimekuwa zikiuzwa kwa bei ya juu.








## Kunenge aipa Rufiji siku 15 majibu hoja za ukaguzi

**Na Julieth Mkireri, RUFIJI**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, ameiagiza Halmashauri ya Wilaya Rufiji kutoa majibu kuhusiana na hoja za ukaguzi wa hesabu ambazo hazijafungwa hadi sasa kabla ya Juni 30.

Alitoa maagizo hayo jana kwenye Baraza Maalumu la Madiwani wa Halmashauri ya Rufiji la kujadili taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/2020.

Taarifa ya maagizo hayo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Kanal Patrick Sawala, kwa niaba ya RC Kunenge.

Alisema kuna baadhi ya hoja ambazo ziko ndani ya uwezo wa halmashauri na hazijafungwa hadi sasa, hivyo zote hizo zinatakiwa kutolewa sababu za kuchelewa kabla ya kuanza mwaka mwingine wa ukaguzi haujaanza.

Alisema hoja hizo zinatakiwa kutolewa maelezo ya kutosha ili mkaguzi wa hesabu azifunge.

Pia aliagiza kuchukuliwa hatua za kinidhamu na zilingane na ukubwa wa hasara kwa mtumishi yeyote aliyesababisha hasara kwa halmashauri.

"Kwenye taarifa yenu nimeona kuna watumishi wamekusanya fedha bila kuzifikisha benki kiasi cha shilingi 189,249,365 ninaagiza fedha hizo zirudishwe kabla ya Juni 30 na watumishi husika wachukuliwe hatua," alisisitiza.

Aliitaka pia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza na kuchukua hatua kwa hoja ambazo hazijafungwa hadi sasa na taarifa ifike ngazi ya mkoa kabla ya Juni 19.

Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Mwanaisha Tumbo, aliwataka watumishi kufuata kanuni, taratibu na kanuni miongozo kuepuka kuibua hoja mpya.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Rufiji, Juma Ligomba, alimwomba Katibu Tawala wa Mkoa huo kufanya utaratibu wa kuongezewa mkaguzi wa hesabu, kwani kitengo hicho kina mtumishi mmoja.

# Mkazi Tunduru alalamika kuvunjiwa nyumba bila fidia

**Na Maulid Mmbaga**

MKAZI wa Kata ya Namakambale, Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Abdallah Kitone, amelalamikia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) kwa kutomlipa fidia baada ya kubomoa nyumba yake.

Akiongea na Nipashe jana, Mikocheni jijini Dar es Salaam, alisema mwaka 2011 maofisa TANROAD waliwataka kubomoa makazi yao ili kupisha mradi wa barabara na wakafanyiwa uhakiki na tathmini ya thamani ya nyumba zao kwa ajili ya fidia, lakini mpaka sasa hajalipwa kwa madai kuwa hajatimiza vigezo.

Akizungumzia madai hayo, Mkurugenzi wa TANROAD, Mhandisi Alinanuswe Kyamba, ambaye alikuwa msimamizi wa mradi huo, alisema wakati walipokuwa wakifanya uhakiki wa kuwalipa watu fidia waligundua kuwa kuna wengine walijiingiza kinyemela na hawakutimiza vigezo vya kulipwa na kutolewa katika orodha na kuwalipa waliokidhi vigezo.

"Wote waliostahili kulipwa walishalipwa na serikali ilishatoa maamuzi kwamba wale wote ambao hawakulipwa hakuna malipo tena ya fidia na waziri alisaini barua, akatuma kwa mkuu wa mkoa huo akawapa wakuu wake wa wilaya, kwa hiyo suala hilo lilikwisha kwa upande wa serikali," alisema.

Pia alisema mwaka 2008 serikali katika jitihada zake za kutunza hifadhi za barabara ilitoa hati za kuwataka wamiliki kubomoa nyumba kwa sababu walivamia barabara na lilitekelezwa, baadaye ulikuja mradi wa wafadhili na walitaka watu walipwe kabla ujenzi haujaanza.

"Sisi tumeshatekeleza siku nyingi hati hiyo na tulitekeleza kwa mujibu wa sheria za Tanzania, na kulikuwa na baadhi ambao nyumba zao zilikuwa hazijabomolewa na wale ambao barabara ilipita sehemu ambazo walipaswa kulipwa hao ndio walilipwa wote.

"Hao wanaodai ni wale ambao walibomoa zamani kabla ya mradi na tulitekeleza kwa mujibu wa sheria kwamba ndani ya mita 22 na nusu hakuna kulipa, na hao ndio walikuja kusema kuwa sisi mbona tulibomoa na hamkutulipa tukawaambia kuwa mlibomoa kwa mujibu wa sheria kwa hiyo hampaswi kulipwa," alisema.

Alibainisha kuwa mwaka 2018, Waziri wa Ujenzi alitoa barua wote ambao wanadai katika barabara hiyo hakuna fidia kwasababu mradi umekwisha na kilichokuwa kinatawaka kulipwa ni kwasababu ya sheria ya wafadhili na kwa kuwa umekwisha wanarudi katika sheria za nchi kuwa ndani ya mita 22 na nusu mtu hapaswi kulipwa fidia hilo ndilo agizo alilolitoa waziri.

Mlalamikaji Kitone alidai kuwa wanachokisema mamlaka husika hakina uhalisia na wanamwomba Makamu wa Rais kuingilia kati suala hilo ili wapatiwe haki yao.

"Sisi tunamwomba Makamu wa Rais aingilie kati, siyo kwamba tunadai tu kwa sababu tunadai, hicho wanachosema si kweli, tuko tayari kukutanishwa nao ili tusikilizwe kama itakuwa kweli hatuna haki basi hatuna shida, ila kama tuna haki basi tupate haki yetu kwa mujibu wa sheria sio kwa kulazimisha," alisema.




Mkuu wa Huduma za Masoko wa Tigo, William Mpinga, akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa kampeni mpya ya siku 90 inayoitwa Cha Asubuhi. Kushoto ni Kaimu Ofisa Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Tigo, David Umoh. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tigo yaja na kampeni mpya ya 'Cha Asubuhi'

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo Tanzania, imezindua kampeni mpya ya siku 90 inayoitwa Cha Asubuhi.

Katika kampeni hii mpya kila mteja anayenunua kifurushi cha kila siku, kila wiki au kila mwezi atapata bonasi ya dakika za bure kupiga Tigo kwa Tigo kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 3 asubuhi.

Mteja wa kifurushi cha kila siku atapata bonasi ya dakika 10 hadi MB 10, wakati mteja wa kifurushi cha kila wiki atapokea dakika 70 hadi MB 700 na mteja wa kifurushi cha kila mwezi atapata dakika 300 hadi GB 3.

Akizungumzia kampeni hiyo jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Ofisa Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Tigo, David Umoh, alisema: "Daima tunatafuta njia za ubunifu za kuwazawadia wateja wetu wenye kazi na kuwafurahisha, kampeni hii inatoa fursa nzuri ya kuungana na wateja wote tuliokuwa nao kwa muda mrefu."

"Tunaamini kuwa mipango mingi hufanywa mapema asubuhi na kwa kuwa tuna nia ya kukidhi mahitaji ya wateja wetu kote nchini. Kampeni hii inawapa fursa watu wanaoamka mapema na wale ambao wanapendelea kupanga shughuli zao za kila siku kuanzia asubuhi," alisema Umoh.

Alisema miaka mingi Tigo Tanzania imekuwa ikianzisha ubunifu kama vile Facebook ya bure kwa Kiswahili, simu mahiri za Kiswahili na vifurushi kama walivyofanya jana. "Mipango yetu ni kuhakikisha tunaondoa vizuizi kwa wateja wetu kwa ajili ya kufanya mawasiliano ya muhimu kupitia kampeni mpya ya Cha Asubuhi. "Zaidi ya wateja milioni 12 wa Tigo wataweza kuamka na kupiga simu za bure, kuperuzi mtandao, bila wasiwasi wa kuwa na muda wa maongezi kwenye simu zao. Hii inadhihirisha juhudi zetu katika kuwa fursa inayowapa wateja wetu huduma bora," alisema Umoh.

## Waziri Aweso atengua Mkurugenzi Maji

**Na Renatha Msungu,**DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amemtengua Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sengerema, Mhandisi Robert Lupoja, huku akimteuwa kushika nafasi hiyo Mhandisi Sadala Sadick Hamis ili kuendelea na majukumu.

Pia ameivunja Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sengerema, ambapo taratibu nyingine za kazi zinaendelea.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na kitengo cha Mawasiliano cha Wizara ya Maji, uteuzi huo unaoanza mara moja, Mhandisi Hamis alikuwa mtumishi katika Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Waziri Aweso amefanya uteuzi huo kwa mamlaka aliyopewa kwa mujibu wa sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na 5 ya 2019.

Taarifa hiyo ilisema kuwa Mhandisi Lupoja ambaye ametenguliwa atapangiwa majukumu mengine ya ujenzi wa taifa.

Kuhusu Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sengerema, taarifa ilieleza kuwa baada ya kuvunjwa kwa bodi hiyo taratibu nyingine za kiofisi zinaendelea kufanyiwa kazi.

## Mtandao wa Airtel kuunganisha miji 400

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania imeanza kuboresha mtandao wake wa 4G ambapo miji zaidi ya 400 nchi nzima itaunganishwa na mtandao wa 'Supa-4G'.

Mtandao wa Airtel Supa-4G unawahakikishia watumiaji huduma zenye ubora wa hali ya juu na wepesi wa kufungua faili.

Kampuni ya Airtel Tanzania hivi karibuni iliboresha huduma zake za mtandao kwa kuwaunganisha wateja wake kutoka miji ya Rufiji mkoani Lindi, USA-River mkoani Arusha na Ilula, Iringa ambao kwa sasa tayari wanafurahia huduma za Supa-4G.

Akizungumza juzi mjini Ilula mkoani Iringa baada ya uzinduzi wa mtandao wa Supa-4G, Meneja Mauzo wa Airtel katika mji wa Ilula, Godfrey Maneno alisema kampuni hiyo ya simu za mkononi ipo katika hatua za kuboresha mtandao wake wa 4G, ikiwa ni moja ya mipango ya muda mrefu ya kuhakikisha inatoa huduma bora za mawasiliano kwa wateja wake nchi nzima.

"Uboreshaji wa mtandao wetu wa mtandao wa 4G ni moja ya mipango mingi ya kuboresha miundombinu yetu ya mawasiliano ili kutoa huduma bora ya mawasiliano kwa wateja wetu wa mijini na vijijini.

Huduma za mawasiliano kwa sasa sio starehe, bali ni hitaji la muhimu," alisema Maneno na kuongeza kuwa kampuni inaamini kuwa wateja watakuwa na uwezo wa kuboresha hali zao za maisha kupitia huduma bora za mawasiliano.

HABARI BUNGENI

# Maboma zahanati kujengwa kwa bil. 28/-

BUNGE limeelezwa kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22, kiasi cha Sh. bilioni 27.75 kimetengwa kwa ajili ya umaliziaji wa maboma 768 ya zahanati kote nchini.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, aliyeaeleza hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Anatropia Theonest.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kutekeleza Sera ya Afya ya kuwa na Kituo cha Afya kwa kila kata ili kupunguza vifo vya mama na mtoto.


Akijibu swali hilo, Dk.Dugange alisema mikakati mingine ya serikali kwa mwaka huo pia kuendelea kujenga vituo vya afya 121.

"Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Afya ya kuwa na zahanati kwa kila kijiji na kituo cha afya kwa kila kata kwa awamu ambapo kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2020/21 serikali imejenga zahanati 1,281, vituo vya afya 488 na hospitali za halmashauri 102," alisema.

Aidha, alisema mpango huo umewezesha kuongeza vituo vya afya katika mamlaka za serikali za mitaa vyenye uwezo wa kutoa huduma za dharura za upasuaji kutoka vituo 115 Desemba 2015 hadi vituo 352, Juni 2021 na hivyo kuchangia katika kupunguza vifo vya wajawazito na watoto.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji lini sera ya serikali kuwa na zahanati kila kijiji na kituo kila kata itatekelezwa ipasavyo.

Naibu Waziri huyo akijibu, alisema mkakati unaendelea kutekelezwa na Kyerwa itapewa kipaumbele ili kurahisisha huduma kwa wananchi.



Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson akiangalia bendera mpya ya Bunge, bungeni jijini Dodoma jana, ambayo baadhi ya wabunge walilalamikia na kuomba mwongozo kuwa ina rangi tofauti zilizopo kwenye bendera ya Taifa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sababu maeneo yenye minara ya simu kukosa mawasiliano yatajwa

IMEELEZWA kuwa kukosekana kwa huduma ya mawasiliano kwenye baadhi ya maeneo yenye minara ya simu ni kutokana na tatizo la kijiografia katika eneo husika.

Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Andrea Kundo, alibainisha hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Urambo (CCM), Magreth Sitta.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni lini kata 16 zisizo na mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Urambo zitapatiwa mawasiliano ya simu na kuwaondolea wananchi adha ya kutokuwa na mawasiliano kwa muda mrefu.

Hata hivyo, alihoji sababu za maeneo yenye minara ya simu kuwa na matatizo ya mawasiliano.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Kundo alisema sababu za kijiografia ya eneo husika zinachangiwa na uwepo wa milima, mabonde na uoto wa asili wenye miti mirefu ambayo huzuia huduma za mawasiliano.

Alitaja sababu nyingine ni kukosekana kwa nishati ya umeme wa uhakika pia inasababisha mnara kushindwa kutoa huduma za mawasiliano.

Awali, alifafanua jimbo la Urambo lina jumla ya kata 18 ambapo kata zote zina huduma ya mawasiliano isipokuwa baadhi ya vijiji katika kata tisa za Kiloleni, Itundu, Imalamakoye, Ugalla, Vumilia, Nsondo na Uyogo. Alisema Kata za Utundu na Ukondamoyo zitafikishiwa huduma za mawasiliano na kampuni ya simu ya Vodacom ifikapo Oktoba, 2021, kata za Nsondo na Uyogo zitafikishiwa huduma za mawasiliano na kampuni ya Airtel ifikapo Oktoba, 2021.

Aidha, alisema kata ya Vumilia itafikishiwa huduma za mawasiliano kupitia kampuni ya simu ya Halotel ifikapo Septemba, 2021 pamoja na kata ya Ugala itakayofikishiwa huduma na kampuni ya simu ya TTCL ifikapo Septemba, 2021.




"Kata za Kiloleni na Imalamakoye zitaingizwa kwenye miradi ya mfuko itakayotekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha," alisema.

# Neema umeme wa uhakika Katavi yaja

SERIKALI imetakiwa kubainisha mipango yake ya kuongeza kasi ya kufikisha umeme wa msongo mkubwa katika Mkoa wa Katavi.

Mbunge wa Mpanda Mjini (CCM), Sebastian Kapufi, alitoa kauli hiyo bungeni alipokuwa akiuliza swali kwa Wizara ya Nishati.

Akiuliza swali, Kapufi alisema kuna hali ya kusuasua katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme.

"Nafahamu utiaji mikataba ya ujenzi haujafanyika naomba serikali inihakikishie lini suala hili litafanyika ili kuharakisha mradi huu," aliomba.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, akijibu swali hilo, alisema serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme wa Gridi ya Taifa wa msongo wa kilovolti 132 yenye urefu wa kilometa 381 kutoka Tabora hadi Katavi na ujenzi wa vituo vitatu vya kupoza umeme vya msongo wa kilovolti 132/33kV Ipole, Inyonga na Mpanda.

Alisema ujenzi wa majengo ya vituo vya kupooza umeme vya Ipole na Inyonga pamoja na uzio umekamilika kwa takribani asilimia 90 na mradi unatarajia kukamilika ifikapo Agosti, 2023 huku gharama ikiwa ni Sh. bilioni 64.9.

Alisema serikali pia inaendelea na taratibu za ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 400 kutoka Iringa, Mbeya, Tunduma, Sumbawanga kupitia Mpanda hadi Kigoma kilometa 1,232.

Aidha, alisema kazi inayofanyika kwa sasa ni kukamilisha taratibu za kupata mtaalamu mshauri wa kuandaa nyaraka za kumpata mkandarasi wa kuanza ujenzi wa mradi.

"Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza Novemba, 2022 na kukamilika mwezi Oktoba, 2024. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 470.42," alisema.



Wakulima walililia Bunge wamechoka na hadaa hizo

Ukurasa 12



Ukurasa 13

**Hedhi inapoendelea kukwamisha wasichana mijini, vijijini kusoma**


# siasa

JUMATANO JUNI 16, 2021

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

PROFESA MWESIGA BAREGU

**Ameondoka kabla ndoto kutimia**

SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# Bajeti 2021/22 imwokoe mtoto na maafa uhaba sugu wa vyoo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI kusoma katika mazingira duni na hatarishi kwa afya zao kutokana na kukosa miundombinu muhimu kama vyoo, limeendelea kuwa tatizo sugu ambalo mzizi wake wataalamu wanautaja kuwa ni bajeti isiyotosheleza.

Ni changamoto inayomkabili mtoto popote bila kujali anasoma kijijini au mjini.

Mkoani Shinyanga, Shule ya Msingi Mwamagunguli 'A' iliyopo Kolandoto Manispaa ya Shinyanga, inapambana na tatizo hilo, kumwezesha mwanafunzi kusoma salama. Inataka kujiondoa kwenye orodha ya shule nyingi zinazokabiliwa na vyoo vibovu vinavyotishia kuzuka maradhi ya mlipuko.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Adam Bega, anaiambia Nipashe wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, anasema shuleni hapo wapo wanafunzi 412, wavulana wakiwa 211, wasichana 201 na walimu nane na wote wanatumia choo kimoja chenye matundu manne.

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu Tanzania wasichana 25 wanatakiwa kutumia tundu moja la choo wakati kwa wanaume ni 26 kwa tundu.

Kwa uwiano huo wanaume 211 wa shule hiyo walihitaji matundu 8 halikadhalika wasichana nao wangepaswa kuwa na vyoo nane.

Wakati shule hiyo ikikabiliwa na changamoto hiyo, Diwani wa Kolandoto Mussa Andrew, anasema tatizo la shule hiyo kutishiwa kufungwa kwa sababu ya choo kujaa na kuchafuka kwa kinyesi ni kazi ya kikwazo cha kwanza alichokumbana nacho alipoanza kazi.

Anasema: "Ilibidi niende halmashauri kuomba angalau choo hicho kizibuliwe, ili wanafunzi waendelee kusoma wakati mipango ya kujenga kingine, ikiandaliwa."



Diwani wa Kolandoto Mussa Andrew (kulia) na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mwamagunguli "A," Adamu Bega, wakitafakari kuboresha choo cha shule ili kuepusha hatari kwa wanafunzi na walimu. **PICHA: MARCO MADUHU**

Andrew anasema choo hicho kilizibuliwa, na wanafunzi wakaendelea kukitumia hivyo hivyo, licha ya kuhatarisha afya zao, ili wasikose masomo sababu ya shule kufungwa kutokana na ubovu wa choo.

"Mikakati iliendelea hadi tukapata wahisani kutoka Shirika la Thubutu Afrika Initiative's likiahidi kutujengea matundu nane kwa ajili wa wasichana ," anasema Andrew.

"Thubutu linatekeleza miradi ya watoto wa kike hapa Shinyanga, ndiyo maana masharti yake ni kuwajengea wasichana choo na chumba maalumu cha kujistiri wakati wa hedhi,"anaongeza Andrew.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwamagunguli, Makoye Shindai, anasema baada ya kupata msaada huo wa wasichana shuleni hapo, alihamasisha wanakijiji kuchangia nguvu kazi ili kuwaunga mkono.

Anasema kijiji kina kaya 580 na wote walishiriki kwenye ujenzi huo wa choo kwa kuchimba shimo, kusomba mawe, mchanga, pamoja na maji kila siku ya ujenzi na kumwagilia jengo," anasema Shindai.

Mwalimu Mkuu Bega anasema choo wanachotumia si imara ni kibovu, kimejaa na licha ya kuzibuliwa, hakifai kwani si salama kwa afya za watumiaji.

**BAJETI ZIJIONGEZE**

"Tulishaandika dokezo Halmashauri ya Shinyanga, kuomba kujengewa choo shuleni hapa, lakini hakuna mrejesho na tunaendelea na kutumia choo hiki hatari kwetu sote,"anasema Bega.

Ofisa Afya Kata ya Kolandoto, Elias Jilala, anasema choo hicho hakifai tena kutumika na kilipaswa kujengwa kingine.

Anaainisha magonjwa kama minyoo, kichocho, kuhara damu, kuharisha, homa ya matumbo pamoja na kipindupindu kuwa yanaweza kuwapata.

Mtendaji wa Kolandoto Wilison Mwakaluba, anasema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, wametoa vipaumbele vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukiwamo ujenzi wa miundombinu ya shule.

Anasema Kolandoto kuna shule za msingi tano ambazo ni Mwamagunguli 'A' na 'B', Galamba, Wame, na Kolandoto, lakini zinachangamoto kubwa ya vyoo, ambazo ni Mwamagunguli 'A' na Kolandoto.

"Katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2021-2022, wametenga fedha kujenga vyoo vya walimu,"anasema Mwakaluba.

Mwanafunzi Naomi Martin, anayesoma darasa la tano Mwamagunguli A, anasema ubovu wa choo shuleni hapo, unawapa hofu ikiwamo ya kupata magonjwa ya mlipuko na ni hatari kwa mazingira kutokana na kuwapo harufu kali.

"Wavulana wanaweza kujisaidia haja ndogo vichakani, shida ina kuja kwetu wasichana hatuwezi kufanya hivyo, lazima tuingie tu chooni licha ya kuwa kibovu na kuhatarisha afya na maisha yetu na kibaya hata maji ya kunawa mikono hakuna,"anasema Naomi.

Daudi Alphonce ni mkazi wa Kolandoto, anayesema kuwapo na tatizo la ubovu wa miundombinu ya vyoo kunakohatarisha afya za watoto wao, wameona umuhimu wa kushiriki kuchangia nguvu kazi ili kumaliza tatizo hilo.

Anasema zamani wananchi hawakushirikishwa kwenye utoaji vipaumbele vya bajeti, na kujikuta wanatekelezewa miradi ambayo siyo vipaumbele vyao, ndiyo maana ilikuwa wagumu kushiriki kwenye utekelezaji wa shughuli za maendeleo hasa ya watoto.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Geofrey Mwangulumbi, anasema katika bajeti ya 2021/2022 wamelenga kukusanya Sh. bilioni 34.1, ambazo zitajenga miundombinu ya shule vikiwamo vyoo.

Mratibu wa mradi wa mijadala jumuishi katika masuala ya kiuchumi, utawala, na fedha, Alex Enoc, kutoka Save the Children, linalotetea haki za watoto, anasema katika Manispaa ya Shinyanga wameendesha mafunzo ya namna ya uundaji wa bajeti jumuishi.

Anasema shirika liliona kuna upungufu kwenye uandaaji wa bajeti za halmashauri, hasa katika kutenga fedha kutekeleza mambo ya watoto likiwamo suala la miundombinu ya elimu na afya likaanzisha utaratibu wa kuhamasisha kushirikisha wananchi.



Mihogo ikiwa imetandazwa chini sokoni. **PICHA: MTANDAO**

# Wakulima walililia Bunge wamechoka na hadaa hizo

**Na Theonestina Kaiza-Boshe**

KWA muda mrefu sasa, Tanzania imekuwa ikiimba wimbo wa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi na kwa nyakati mbalimbali serikali imetengeneza sera na kaulimbiu za kuchochea dhana hiyo.

Aidha, ilifikia wakati serikali ikaja na mkakati na kaulimbiu ya "Siasa ni Kilimo". Ama kwa uhakika juhudi nyingi zimefanywa katika azma ya kuinua kilimo, sambamba na kuondoa umaskini nchini.

Lakini kinachoshuhudiwa ni matokeo yasiyolandana na nguvu na kauli zinazoelekezwa kwenye kilimo kwa sera, kaulimbiu na programu maalum.

Kwa ujumla mavuno na kipato kitokanacho na kilimo mashambani na vijijini hayaendani na juhudi za kuhimiza kilimo.

Hotuba ya bajeti ya 2020/2021 inasema kilimo kimeendelea kutoa ajira kwa Watanzania takribani asilimia 58 na kuchangia asilimia 28.2 ya pato la taifa, aidha iliainisha kuwa ukuaji wake kati mwaka 2015 na 2019 ni wastani wa asilimia 5.2 na ukuaji huu unaelekea kutokana na mazao ya maua, matunda na mboga, ambayo miaka ya nyuma hayakuwa ya biashara.

Hivyo, mchango huo wa kilimo unaoonekana sasa unatokana zaidi na idadi ya wakulima na mazao mapya mchanganyika na si kutokana na ongezeko la tija kwa mazao makuu yanayolimwa

> Walikuwa wananunua makopa (muhogo mkavu) kwa Sh. 300 kwa kilo na kwamba mkulima au muuzaji alitakiwa kuwapelekea kwa gharama zake na kama wataridhika ndipo wanunue.

na wakulima walio wengi.

Mambo yanayosababisha hali hiyo yamejadiliwa mara nyingi na mikakati ya kukabiliana na hali hiyo kutajwa.

### KILIO CHA WAKULIMA

Wakati bajeti ikiendelea jijini Dodoma, ni wakati wa kuziangalia fursa mpya za kimataifa zinazoweza kumuinua mkulima na taifa likanufaika kiuchumi haya ni masoko ya nje yaliyoelezwa kuwa Tanzania imeingia mikataba.

Kwa mujibu wa taarifa zinazozungumzia fursa hizo kuna nchi zinahitaji kiasi kikubwa cha mahindi ya njano, ufuta na muhogo kiasi kwamba, kwa kuanzia, Tanzania haiwezi kukidhi mahitaji ya masoko hayo kwa mazao yaliyotajwa. Aidha, kwa kiasi kinachohitajika, serikali ikitimiza wajibu wake barabara, zao moja, au mawili, yanaweza kuinua maisha ya wakulima wengi na kuongeza pato la taifa kwa kiwango kikubwa sana.

Lakini, kwa kile kilichoonekana kwenye mkataba wa fursa za kibiashara kati ya Marekani na Afrika wa AGOA na ule China na biashara ya muhogo mwaka juzi, wakulima wa kawaida wanaweza wasiambulie chochote.

Mathalani, mkataba wa muhogo na China, kiliibuka kizungumkuti Wizara ya Kilimo, kinachohitaji kutanzuliwa, kama serikali inataka kumwinua mkulima na kukuza pato la taifa kutokana na fursa kubwa za masoko ya mazao ya kilimo nje ya nchi.

### KILICHOWASIBU WAKULIMA

Wanaolima muhogo baada ya kujua kulikuwa na soko kubwa China na kuhimizwa kuzalisha kwa wingi, wengi walioathiriwa na kizungumkuti hicho.

Baada ya msimu kuanza wakiwa na taarifa za mkataba huo wa soko la muhogo mbichi China, walianza kutafuta taarifa wizarani kutaka kujua utaratibu.

Japo walipatiwa mawasiliano na mratibu wizarani, hakukupatikana na taarifa nyingine zilizotolewa zilikuwa za kukatisha tamaa.

Kwa mfano, yaliwahi kutolewa maelekezo ya kumtafuta mnunuzi wa mihogo Kiwangwa Bagamoyo, ambaye alikuwa Mtanzania na si kampuni za China, aliyekuwa akinunua muhogo mbichi kwa Shilingi 100 kwa kilo. Aidha, alikuwa afikishiwe kiwandani kwake.

Wizara haikutoa taarifa za wafanyabiashara Wachina waliokuwa wananunua muhogo na wakati mmoja kulikuwa na taarifa ya kuwa kulikuwa Wachina Mtaa wa Zanaki na Bibi Titi Mohamed jijini Dar es Salaam, waliokuwa wananunua makopa safi.

Walikuwa wananunua makopa (muhogo mkavu) kwa Sh. 300 kwa kilo na kwamba mkulima au muuzaji alitakiwa kuwapelekea kwa gharama zake na kama wataridhika ndipo wanunue.

### SOKO BURUNDI

Kingine cha kushangaza, ni wakulima kushauriwa kusindika muhogo na kujaribu soko la Burundi, hapo ndipo kizungumkuti. Kwa maana wakati huo huo kuna matukio matatu yaliyowachanganya.

Tukio la kwanza ni la taarifa za Wachina waliokuwa wananunua muhogo Dar es Salaam, halafu baadaye wakadaiwa wamekwenda Tanga bila taarifa za mahali walikokuwa wanapatikana au namna ya kuwasiliana nao. La pili ni kuona kwenye vyombo vya habari Wachina fulani wakitoa mashine za kuchakata muhogo kwa Mkuu wa Wilaya Handeni, Tanga.

Tukio la tatu ni wakati wakulima wakizidi kuwa na maswali kuhusu mradi huo wa muhogo na wanunuzi wa China, vyombo vya habari vilichapisha taarifa ya mfanyabiashara mashuhuri nchini kupeleka shehena kubwa la muhogo China.

Wakati hayo yote yanaendelea, muhogo shambani uliishakomaa na kuanza kuhabirika walioweza walichakata na kusindika unga na kutafuta soko la ndani la bidhaa hiyo, ambayo ilikuwa ni kazi ngumu, vile soko linatakiwa kulitafuta kabla hata ya kulima.

Hata hivyo mihogo iliyo mingi iliharibikia mashambani na kukatisha wakulima tamaa.

Ombi la wakulima kwa serikali na bunge linalojadili bajeti Dodoma ni kutatua kero kuhusu mikataba ya kimataifa ya masoko ya mazao inayoonekana wizara ya Kilimo na wadau wengine kama ile ya Viwanda na Biashara na kuwawezesha wakulima kupata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu masoko ya mahindi ya njano, ufuta na muhogo.

Aidha ichunguzwe na kufahamika kwa nini wakulima hapa nchini hawajaweza kunufaika na AGOA, kwa lengo la kurekebisha mambo yaliyosababisha hali hiyo kwa muda wa zaidi ya miaka 20 sasa.

SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# Hedhi inapoendelea kukwamisha wasichana mijini,vijijini kusoma

• Bajeti ifute kodi zote taulo za kike

**Na Gaudensia Mngumi**

MTOTO wa Afrika akiwamo binti wa Tanzania anaendelea kuzungukwa na majanga na leo, karne ya 21, anashindwa kusoma kwa sababu hana taulo za kike wala hafahamu kuhusu hedhi.

Changamoto hii inabuliwa wiki hii wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, kukiwa na taarifa kuwa idadi kubwa ya wasichana hasa wa jamii za wafugaji wanakatisha masomo wanapoanza kupata hedhi, kwa vile hawafahamu ni kitu gani.

Kukosekana elimu na ufahamu wa mabadiliko hayo yanayotokea kwa wanawake baada ya kupevuka , kunawatisha wasichana na baadhi wanadhani kuwa ni ugonjwa.

Ni kwa mujibu wa utafiti wa shirika lisilo la kiserikali la Usawa wa Wanawake na Wasichana (FOEPA), lililofanya uchunguzi mkoani Kilimanjaro hivi karibuni.

Mkurugenzi wa FOEPA, Janeth Shirima, anasema katika utafiti huo wanabaini kuwa, wanafunzi wengi wasichana walio katika umri wa kupevuka, wanakatisha masomo wanapopata hedhi, wakijihofia kuwa wamepatwa na ugonjwa.

Anasema pamoja na utafiti huo kuchukua sehemu ndogo ya Tanzania ni wazi kuwa huenda ukosefu wa elimu ya hedhi umekuwa tatizo kwa mabinti wengi na huenda pia umewakwamisha kielimu.

Kinachowatatiza ni suala la siku za mwezi kubaki kuwa siri, mwiko na mambo yasiyozungumzika kwenye jamii nyingi.

Wakati dunia inapoadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika leo , sintofahamu ya hedhi salama, ufahamu duni wa hali hiyo, mimba za utotoni na unyanyasaji wa wasichana umekuwa giza nene linalowakwamisha mabinti kusonga mbele kwa karibu kila sekta.

Mambo hayo yanawazuia kusoma na kufikia malengo wanayoyakusudia, yanawakwamisha kuendelea na elimu ya sekondari na ya juu na hata kupata kazi zenye staha.

Wakati akizungumza na wanawake mkoani Dodoma wiki iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan, anasema idadi ya watoto walioko katika shule za msingi nchini ni takribani milioni 11, wasichana wakiwa ni 560,000 kiwango hicho kikikaribiana na wavulana.

Lakini, takwimu za Rais zinazidi kupungua na upungufu unaanza kuonekana kwenye sekondari hadi vyuo vikuu idadi yao ikizidi kushuka.

Anataja elimu ya sekondari kwa kidato cha sita kuwa idadi ya wanafunzi ni 160,461 na kati yao wasichana ni takribani 70,000 na katika vyuo vikuu wasomi wako 267,000 na wasichana ni 88,579.

Kwa mujibu wa Rais idadi ya wanawake inashuka wanavyozidi kupanda ngazi kimasomo jambo analoahidi serikali yake italifanyia uchunguzi na kulitolea maelezo.



Wasichana wanaelezwa umuhimu wa kusonga mbele kitaaluma ndio mkombozi wa maisha yao. Bajeti inayojadiliwa sasa ianze kutatua matatizo yao. **PICHA: MTANDAO**



Wakati huu tafakari ya Mtoto wa Afrika ikiendelea miongoni mwa wadau, eneo mojawapo linawakwamisha mabinti kusoma na hata kuacha shule ni ukosefu wa taulo za hedhi.

Si hivyo tu, hata pale serikali ilipoondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kwenye pedi ilipowasilisha bajeti ya mwaka jana (2020/21) ambao unamalizika mwisho wa mwezi huu, pedi zimeendelea kuuzwa ghali kupindukia.

Akitoa maoni yake Zainab Ismail, anasema pedi zinauzwa ghali kiasi kwamba wanawake wasio na kipato rasmi hawawezi kumudu gharama hizo.

"Kama mama hawezi kununua taulo kila mwezi binti zake wanaosoma shule za msingi na sekondari watazipataje?" Anahoji na kushauri serikali wakati huu wa mjadala wa bajeti kuchunguza kwa kina ni kitu gani kinachosababisha pedi kuuzwa bei juu wakati zimepunguziwa kodi?

> Mambo hayo yanawazuia kusoma na kufikia malengo wanayoyakusudia, yanawakwamisha kuendelea na elimu ya sekondari na ya juu na hata kupata kazi zenye staha.

Kwa mujibu wa maelezo ya Zainab mmiliki wa duka lililoko Salasala jijini Dar es Salaam, pedi huuzwa kati ya Shilingi 2,000 hadi 5,000 hata kama zimezalishwa nchini na ndiyo bei iliyoko kwenye maduka ya dawa na vipodozi, ya shule na sehemu zote mitaani pamoja na vijijini.

Anakumbusha kuwa malengo yaliyokuwa yakipigiwa kelele na watetezi wa wasichana akiwamo mbunge Upendo Peneza ni kwamba zinapaswa kupatikana kwa uhakika na zinaweza kununuliwa na watumiaji wote walioko mijini na vijini pengine kwa gharama ya Sh. 500 hadi 1,000.

Anasema kwa sasa bado wengi hawawezi kuzinunua kutokana na bei yake kuwa kubwa na jamii nyingi kukosa kipato cha kujikimu kwenye mahitaji muhimu hivyo taulo hizo kukosa kipaumbele, anasema.

Hata sasa wanafunzi wa msingi na sekondari wanalazimika kukatisha masomo na kubaki nyumbani kipindi cha hedhi kutokana na kukosa taulo za kike na kuepuka aibu shuleni.

**AFRIKA MASHARIKI**

Katika ukanda huo tatizo la hedhi limeendelea kuwasumbua wanawake na wasichana wengi lakini juhudi zimefanyika kupunguza na kuondoa kodi kwenye bidhaa hizo.

Kwa mujibu wa BBC maduka katika mji mkuu wa Rwanda Kigali na kwengineko

**INAENDELEA UK.14**

JUKWAA LA UONGOZI

PROFESA MWESIGA BAREGU

# Ameondoka kabla ndoto kutimia

• Ni ya vijana wajeuri, wakosoaji



Profesa Baregu katika shughuli za kitaaluma na kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

CHADEMA na Watanzania wakiwamo wasomi, wapenda demokrasia na taifa kwa ujumla wapo katika maombolezo ya kifo cha mwanasiasa mbobezi na mwanazuoni Profesa Mwesiga Baregu, aliyefariki mwishoni mwa wiki iliyopita.

Ni mwanasiasa msomi aliyekuwa na matamanio ya kuona nchi inakuwa na vijana wengi 'jeuri' kifikra na wenye uwezo wa kuhoji pale wanapoona mambo yanakwenda segemnege au shaghalabaghala kwa maslahi ya taifa.

Msomi huyo, wakati wa uhai wake aliamini kuwa, vijana wa aina hiyo ni wachache, hivyo kila alipopata nafasi ya kuzungumza ndani ya nje ya chama, aliongea zaidi umuhimu huo ili taifa lisiwe la watu wanaosema 'ndiyoooo' kwa kila jambo.

Katika moja ya mazungumzo yake na gazeti hili, Profesa Baregu anasema; " Tunahitaji kuwa na vijana 'shinikizi,' kuwa na vijana 'jeuri', wenye uwezo wa kuhoji na siyo wanaoitikia ndiyo kila kitu, lakini pia watafutaji na wanaojishughulisha" Prof. Baregu aliwahi kusema.

> Alikuwa ni mmoja wa wajumbe waliokuwamo kwenye Tume ya Jaji Warioba iliozunguka nchi nzima kukusanya maoni ya wananchi kuhusu kuwapo kwa katiba mpya.

### KWANINI ALIHISI HIVYO?

Msomi huyo wa sayansi za siasa anabainisha kuwa taifa lina vijana wengi waoga hawawezi kuhoji chochote na mara nyingi kazi yao imebakia kusifia hata mambo yasiyo na tija na kwamba ili kuondokana na hali hiyo, ipo haja ya kuwaandaa vizuri, wawe watu wa kujiamini na kujenga hoja.

Imani yake ilikuwa ni kwamba, ili kujenga taifa la watu wanaojitambua, suala la kuiambia ukweli serikali ni kipaumbele.

Alisisitiza kuwa kunahitajika wakosoaji wengi zaidi bila kujali itikadi za vyama bali kwa kuzingatia Utanzania na maendeleo ya nchi.

Msomi huyo aliamini kuwa, taifa halitakiwi kuwa na vijana wasio na maono, wanaojipendekeza kwa wakubwa hasa viongozi wa kisiasa ili wajaze matumbo yao, wavivu wa kufikiri na wa kujitegemea wa kutafuta mkate wao.

### MUUMINI WA NYERERE

Profesa Baregu ambaye aliwahi kukitumikia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam lakini pia mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA aliyeshiriki kwenye harakati za ukombozi kusini mwa Afrika nchini Zimbabwe, aliamini kuwa wasomi hawapaswi kujitenga na siasa.

Aliwahi kusema kuwa hata Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alisisitiza kuwa Tanzania inahitaji vijana jeuri, wanaoweza kuhoji na kukosoa, siyo wale ambao ni waoga wa kizazi cha 'ndiyo bwana mkubwa' na kupiga makofi kila wakati.

Hiyo, ndiyo ndoto ambayo mtaalam huyo wa sayansi ya jamii, siasa, utawala na historia ndani na nje ya vyuo vikuu ameondoka nayo akitamani itimie ili Tanzania iwe na vijana wengi na wenye wa kujenga hoja na kuhoji pale anapoona kuna jambo halijakaa sawa.

### BAREGU ALIKOPITIA

Profesa huyo ambaye katika uhai wake, amefanyakazi katika vyuo vikuu mbalimbali nchini, kikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na alipostaafu akaenda Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania (SAUT) kilichoko Mwanza, ameacha alama pia kwenye kuchagua na kuamua.

Msomi huyo aliamua kufundisha zaidi UDSM badala ya kuwa Balozi wa Tanzania nchini Italia, baada ya uteuzi aliomba radhi kuwa angependa kuendelea kufundisha kuliko kuwa balozi ughaibuni.

Akiongozwa na imani kuwa huwezi kutenganisha elimu au usomi na siasa, mwaka 2005, Profesa Baregu alijitosa kuchukua fomu ya kuwania urais kupitia CHADEMA, lakini baadaye akaamua kujitoa kwenye kinyang'anyiro hicho na kumwachia Freeman Mbowe awanie.

Vilevile, alikuwa ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, aliyejizolea umaarufu mkubwa ndani na nje ya nchi kutokana na ushiriki wake kwenye mijadala mbalimbali ya kisiasa nchini.

Alikuwa pia mchambuzi wa siasa za kimataifa, ambaye alitumiwa na vyombo mbalimbali vya habari vya ndani na nje ya nchi kuchambua hali ya kisiasa ya nchi yoyote ile ambayo alihitajika kutoa maoni yake.

Aidha, Profesa Baregu pia alikuwa ni mmoja wa wajumbe waliokuwamo kwenye Tume wa Jaji Warioba iliozunguka nchi nzima kukusanya maoni ya wananchi kuhusu kuwapo kwa katiba mpya.

### MJENZI WA DEMOKRASIA

Licha ya Profesa Baregu kuwa mhanga wa kufukuzwa kazi kwa sababu ya kujiingiza kwenye siasa wakati ni mtumishi wa serikali, aliendelea kuamini kuwa wasomi wana mchango kwenye kufundisha vyuoni na kwenye kuendeleza siasa na demokrasia majukwaani.

Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, anasema, mchango wa Profesa Baregu katika ujenzi wa demokrasia nchini ulikuwa ni mkubwa, hasa katika mchakato wa katiba ambayo yeye alikuwa mmoja wa wajumbe wa Tume ya Kukusanya Maoni ya Wananchi.

Prof. Baregu alikuwa mwanazuoni mahiri, msomi uliyeelimika, mwerevu na mfuasi-mchambuzi wa imani za Karl Marx, Thomas Hobbes, Frederick Angels, John Locke, Marchieveli na wengineo," anasema Zitto.

Anasema, mwanazuoni huyo alielewa ni wapi nchi ilipo katika siasa na alielewa pia mwelekeo unaotakiwa kufuatwa ni upi ikiwa kweli Tanzania ina dhamira njema ya kisiasa ya kujenga taifa lisilomilikiwa na dola.

## Hedhi inapoendelea kukwamisha wasichana mijini,vijijini kusoma

**INATOKA UK.13**

nchini humo bei ya paketi moja ya taulo za hedhi, huuzwa kati ya Franga za Rwanda 900 hadi 1000 ambayo ni kama nusu ya dola au Shilingi 1,200 za Tanzania.

Rwanda iliondoa ushuru wa VAT wa Franga 200.

Nchini Kenya pia VAT iliondolewa lakini athari za hatua hizi bado watumiaji hawajazihisi kama ilivyo kwa Tanzania kwa sababu bei bado ni kaa la moto.

Hata hivyo pamoja na taulo za kike kumvuta nyuma msichana anayetaka kusoma, juhudi za kumsaidia binti wa Afrika kusoma na kufikia viwango vya juu, bado zinakumbana na matatizo lukuki.

Kukosekana mabweni kunasababisha wasichana kupewa lifti na madereva wa bajaji na bodaboda kisha kupata mimba lakini wakati mwingine, ukosefu huwalazimisha kuishi mitaani na kubakwa na wanaume wanaowalaghai kwa kisingizio cha kuwahudumia na kuwawezesha kujikimu.

### NAFASI YA BAJETI

Bajeti ya mwaka huu imeonekana kuwa na malalamiko hasa kwa upande wa kubaki kimya kwenye eneo la ujenzi wa mabweni ya wasichana ambao wamekuwa waathirika wa ujauzito utotoni kutokana na kutembea umbali mrefu kufika shuleni.

Ikiwezekana bajeti iliyoondoa kodi kwenye nyasi bandia, iirejeshe ili kupata fedha za kujenga mabweni ya wasichana na kumuokoa binti wa Tanzania.

Aidha, ili kusaidia kupata fedha za kujenga mabweni hayo na kufuta kodi zote kwenye taulo za kike, serikali iendelee kutoza kodi kubwa kwenye pombe na hata bidhaa za tumbaku ili kupunguza matumizi ya pombe na sigara ambayo yana athari kiafya hasa kuchangia ongezeko la saratani nchini.



## HABARI DODOMA

# Serikali yazindua vituo vya malezi

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

SERIKALI imezindua vituo vya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto vinavyolenga kutoa huduma jumuishi kwa watoto walio na umri kuanzia miaka miwili hadi miaka mitano.

Vituo hivyo vitasaidia kuwajenga watoto utimilifu wao ikiwa ni pamoja kuwapatia huduma jumuishi za afya, lishe, ulinzi, kujifunza na uchangamshi wa awali kabla ya kujiunga na darasa la awali wanapofikia umri wa miaka tano.

Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Mwanahamisi Ali Khamis, alibainisha hayo jana wakati akizindua moja kati ya vituo 30 vya malezi, makuzi na maendeleo ya awali katika kijiji cha Chamwino, Ikulu ambacho kimejengwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Shirika la BRAC.

"Kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru wadau wetu wa Maendeleo Shirika la BRAC Tanzania kwa kushirikiana na serikali kujenga vituo 30 vya mfano kikiwemo kituo hiki ambavyo vipo katika hatua tofauti za ujenzi katika halmashauri sita," alisema.

Alisema kuwa huduma hizo zinamwezesha mtoto kukua kimwili, kiakili, kisaikolojia na kimaono akiwa angali mtoto.

Vilevile, alisema hali hiyo itasadia kuwa na taifa lenye watu walioandaliwa kikamilifu kulitumikia.

"Pamoja na faida atakayoipata mtoto moja kwa moja, faida nyingine ya uwepo wa vituo hivi kutatoa fursa kwa wazazi na walezi kupata muda wa kutosha kwa ajili ya kufanya shughuli za maendeleo ya watoto wakiwa vituoni na pia kuwaepusha watoto na hatari mbalimbali ambazo zinaweza kutokea wanapoachwa nyumbani bila uangalizi wa kutosha.

Alisema kuwa mtoto asiyepitia katika vituo vya malezi na makuzi ya awali atakuwa tofauti na aliyepitia kwenye vituo kwa kuwa ataimarika katika stadi za kujifunza, ubunifu na uchangamshi kabla ya kujiunga na darasa la awali.

Alisema watoto wengi hasa wa vijijini ambako hakuna vituo vya malezi wanakosa huduma muhimu za malezi na misingi inayofaa katika maandalizi ya awali ya malezi na makuzi ya mtoto na kuwafanya baadhi ya wanaomaliza darasa la saba kuwa na uwezo na ubunifu mdogo na hata baadhi yao kumaliza shule wakiwa hawajui kusoma au kuandika.

"Uwepo wa vituo hivi unakwenda kumaliza changamoto hizo," alisema.

Pia, alisema kuwa kutokana na manufaa hayo, serikali kwa kushirikiana na wadau wa wa maendeleo itaendelea kuhamasisha na kuamsha ari ya wananchi ili kushiriki katika ujenzi wa vituo hivyo katika vijiji na mitaa yote nchini ili kuhakikisha kuwa huduma hiyo inapatikana.

Hatua hiyo pia itawezesha watoto wote kupitia hatua hiyo ya msingi ya malezi na makuzi kabla ya kuingia kwenye mfumo rasmi wa elimu.

Kadhalika, ujenzi wa vituo hivyo umekuwa ni shirikishi kati ya serikali, wadau na wananchi wa maeneo husika.

"Ni mategemeo yangu kwamba, serikali kupitia halmashauri zote nchini tutaendelea kuhamasisha, kuratibu na kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa vituo hivyo kwa kushirikisha wazazi, walezi na jamii kwa ujumla. Aidha wizara itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo kuanzisha vituo hivi," alisema.

Aliwaomba wadau wote wa maendeleo kushirikiana na serikali katika uanzishaji wa vituo hivyo maeneo wanayofanya kazi ili kuhakikisha kila kijiji na mtaa kunakuwa na kituo cha aina hiyo.

Naye, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la BRAC Tanzania, Susan Bipa, alisema kuwa shirika hilo lilianza kujikita katika sekta ya elimu kwa watoto wadogo kupitia mradi wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya awali ya mtoto mwaka 2016 chini ya ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo wa LEGO.

"Mradi huo unaojulikana kama BRAC PlayLab, umekuwa ukitekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam na Mbeya ambapo vituo 80 vilitumika kutoa mafunzo kwa watoto zaidi ya 3,600 ambao walihitimu miaka miwili ya mafunzo na asilimia 96 ya watoto hao kuingia katika shule za awali kwenye maeneo husika," alisema.



Mwalimu Paul Wadugu kutoka Kanisa la Viziwi la Betheli Baptisti Tanzania (KVBBT), akitoa mafunzo kwa watumishi wa sekta ya afya jijini Dodoma jana, kuhusu mawasiliano ya lugha ya alama zinazotakiwa kutumika kwa watu wenye ulemavu wa kusikia. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC Mtaka atafuta njia kuwezesha wafugaji

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amesema anajipanga kukutana na uongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kujadili namna ya kuwawezesha wafugaji wa mkoa huo kunufaika na shamba la mifugo la serikali lililopo wilayani Kongwa.

Mtaka aliyasema hayo mwanzoni mwa wiki wakati akifungua mkutano wa wafugaji wa mkoani humo.

Alisema, kipaumbele chake katika sekta ya ufugaji kwenye Mkoa wa Dodoma ni kuendesha ufugaji bora, wakisasa, wenye tija na uwekezaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa, ngozi, pembe na kwato.

Alisema atazungumza na wizara hiyo ili wawapatie wakulima wa Dodoma, vitalu vya ardhi kwenye shamba hilo la mifugo la serikali lenye ukubwa wa hekta 38,000 kwa utaratibu wa kukodisha ili wakulima hao wapate maeneo ya kutosha ya kuendeshea shughuli za ufugaji wa kisasa na uoteshaji malisho ya mifugo.

Awali, akisoma risala ya wafugaji, Katibu wa Chama cha Wafugaji mkoani humo, Reginaldo Lubeleje, alisema wanakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo ukosefu wa maeneo ya kufugia, malisho na kwamba maeneo mengi yaliyopo yana migogoro ya mipaka.

Pia, ukosefu wa mipango ya matumizi bora ya ardhi, huduma muhimu kama maji na majosho ya kuogeshea mifugo.

"Baadhi ya maeneo ya ufugaji na malisho yamekuwa yakivamiwa kwa shughuli za kilimo, wakulima bado wana ukosefu wa elimu ya kutosha ya ufugaji bora, hapa Dodoma lipo shamba kubwa la mifugo la serikali wilayani Kongwa, lakini halina mchango katika kuwasaidia wakulima wa Dodoma na kubadili aina ya ufugaji wao kuwa ufugaji bora na wa kisasa," alisema.

# Maofisa waagizwa kuboresha mabaraza ya vijana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAOFISA wa Maendeleo ya Jamii wametakiwa kuhakikisha mabaraza ya watoto nchini yanaimarishwa, huku wazazi na walezi wakiombwa kuwaruhusu watoto kujiunga.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, anayeshughulikia Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Mwanaidi Ali Khamis, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua Baraza la Taifa la Watoto.

Aliwataka kuimarisha mabaraza hayo ili kuhakikisha mambo ya watoto yanazungumzwa pamoja na kutafutiwa suluhu.

"Nitoe wito kwa wazazi na walezi kuwaruhusu watoto kujiunga katika mabaraza hayo ili waweze kupata sauti kwenye mambo yao," alisema.

Alisema kero za upatikanaji wa bima, serikali itazifanyia kazi kwa mujibu wa sheria za nchi huku akiahidi kuwa serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa watoto kuhusu mambo yao.

Awali, Makamu Mwenyekiti wa baraza hilo anayemaliza muda wake, Aidath Ishulula, akisoma risala kwa niaba ya watoto nchini, alisema wanakabiliwa na kero za rasilimali fedha katika kuendesha mabaraza, watoto kutokuwa na bima na kutokukamilika kwa mpango kazi.



# TARI yapania kuinua kilimo cha karanga

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

SERIKALI kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Naliendele mkoani Mtwara, imeanza mikakati ya kuinua kilimo cha karanga kwa lengo la kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kupikia unaolikabili taifa kwa sasa.

Mratibu wa Programu ya Utafiti wa Mbegu za Mafuta nchini, Joseph Nzunda, aliyasema hayo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mkulima wa Karanga yaliyofanyika katika Kijiji cha Ipapa, Kata ya Ipunga, Mbozi mkoani Songwe.

Alisema mbali na kukabiliana na uhaba wa mafuta nchini, pia lengo la serikali ni kuongeza tija kwenye kilimo cha zao hilo ili kuinua kipato cha mkulima na serikali kwa kuongeza uzalishaji utakaoongeza mauzo ya karanga.

Pia alisema serikali inalenga kuboresha lishe kwa wananchi ili kukabiliana na tatizo la udumavu linaloikumba mikoa mbalimbali ikiwamo ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo inazalisha chakula kwa wingi lakini bado tatizo hilo liko juu kuliko kiwango cha kitaifa.

"Tunataka kuongeza tija kwa maana ya kwamba katika eneo dogo ulilonalo mkulima, utumie mbinu za kisasa kuzalisha. Utumie mbegu bora ambazo zimefanyiwa utafiti ili upate mazao mengi. Kwa sasa nchi yetu inakabiliwa na uhaba mkubwa wa mafuta, sasa hii ni fursa kwetu wakulima wa karanga," alisema Nzunda.

Aliwataka wananchi kutumia fursa ya uwapo wa watafiti kujifunza mbinu bora za kilimo ili waachane na kilimo cha mazoea ambacho huwapatia mazao ya kujikimu badala ya kuzalisha kibiashara.

Ofisa Utafiti wa Kituo cha TARI Naliendele, Athanas Minja, alisema tayari ugunduzi wa mbegu bora za karanga umeshafanyika kwa kuzingatia mazingira mbalimbali ya nchi kulingana na hali ya hewa na uwezo wa kuhimili visumbufu.

Alisema kwa sasa wamegundua mbegu zinazokomaa haraka kwa ajili ya kulimwa katika mikoa inayopata mvua za wastani ikiwamo mikoa ya Kanda ya Kati na kwamba mbegu hizo zinakomaa baada ya siku 90 mpaka 100.

Minja alisema baadhi ya mbegu ambazo zinachukua muda mrefu wanahamasisha zilimwe katika mikoa inayopata mvua nyingi ili zisiharibike kwa kushindwa kukaushwa vizuri wakati wa mvua.

"Hizi mbegu ni nzuri kwa sababu zinahilimi magonjwa na visumbufu vingine vya mimea, hivyo tunawashauri wakulima waachane na mbegu za kienyeji ambazo wamekuwa wakizitumia na watumie mbegu hizi bora ili waongeze tija," alisema Minja.

Alisema katika utafiti mbalimbali waliofanya wamebaini kuwa mkoa wa Songwe ni miongoni mwa mikoa ambayo ardhi yake inafaa kwa kilimo cha karanga ndiyo maana wameongeza nguvu ya kuhamasisha wakulima.

## RC aweka mtegoni watendaji wa vijiji

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewapa wiki moja maofisa watendaji 18 wa vijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuwasilisha serikalini fedha walizokusanya kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato lakini wamekaa nazo.

Maofisa hao wanadaiwa kukusanya fedha za serikali zaidi ya Sh. milioni 70 lakini hawajaziwasilisha kwenye akaunti za halmashauri hiyo hali ambayo inatia wasiwasi kwamba huenda wamezitafuna.

Akizungumza juzi wakati wa Kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Homera aliliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata na kuwapeleka selo watendaji hao endapo hawatawasilisha fedha hizo kuanzia Jumatatu ya wiki ijayo.

Pia aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwafuatilia maofisa hao endapo hawatawasilisha fedha hizo na kwamba watatakiwa kuhojiwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Mmejitahidi sana kujibu hoja za CAG lakini lazima hatua zichukuliwe dhidi ya hawa watendaji, leo wamekusanya zaidi ya milioni 70 wamekaa nazo tusipochukua hatua mapema watakuja wakusanye milioni 500 baadaye bilioni moja, sasa ni lazima tuwawahi," alisema Homera.

Aliwapiga marufuku watendaji wa vijiji na kata kutumia fedha mbichi ambazo wanakusanya na badala yake wanatakiwa kuzipeleka halmashauri ili zikapangiwe matumizi kwa mujibu wa sheria.

Aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa huo kuchukua hatua dhidi ya watendaji wanaotumia fedha mbichi na kwamba ikiwezekana wafukuzwe kazi na kuajiri wengine waaminifu.



Wakazi wa eneo la Ilomba, jijini Mbeya, wakiangalia mwili wa kijana mmoja (uliofunikwa na shuka), mkazi wa eneo hilo aliyedhaniwa kuwa amefariki dunia ambapo baadaye ilibainika kuwa ni mzima baada ya kuzinduka wakati maofisa wa Jeshi la Polisi wakimpeleka katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wajasiriamali wataka busara wakati wa utatuzi migogoro

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

SIKU moja baada ya mgogoro kati ya wajasiriamali wa eneo la Kiwira katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya na serikali kumalizika, wajasiriamali hao wameiomba serikali kuheshimu makubaliano waliyofikia na kutumia busara wakati utakapofika wa kuondolewa badala ya kutumia nguvu.

Kwa muda mrefu kulikuwa na mgogoro baina ya wajasiliamali na serikali kutokana na wajasiliamali hao kufanyia kazi zao kwenye eneo ambalo usalama wake ni mdogo, hivyo serikali kuwataka waondoke huku wao wakigoma kwa madai ya kutotengewa eneo la kufanyia biashara zao. Hivi karibuni, serikali ilitumia nguvu kuwaondoa wajasiliamali hao kwenye eneo hilo hali iliyozua vurugu kwa wajasiriamali hao kufunga barabara Kuu ya Tanzania na Malawi kwa kutumia mawe na meza walizokuwa wanafanyia biashara mpaka Jeshi la Polisi lilipoingilia kati.

Hata hivyo, mwishoni mwa wiki iliyopita, uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe alifanya mkutano na viongozi wa wajasiriamali na kukubaliana kuwaacha waendelee na shughuli zao mpaka serikali itakapowatafutia eneo mbadala la kufanyia kazi zao.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wajasiriamali hao walisema kwa muda mrefu wamekuwa wakisumbuana na serikali kuhusu eneo hilo lakini hakuna mwafaka wa kudumu, hivyo wakawaomba watendaji wa serikali kuheshimu makubaliano ya sasa.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Esther Nyabula, alisema kabla ya kufikia makubaliano ya mwishoni mwa wiki, maofisa wa serikali wamekuwa wakiwanyanyasa kwa kuwashurutisha kuondoka bila kuwaonyesha eneo wanalotakiwa kufanyia shughuli zao.

Alikiri kuwa eneo hilo ni hatari kwa maisha yao lakini hawana namna kutokana na hali ya maisha kuwa ngumu, hivyo akasisitiza kuwa wamekuwa makini wanapofanya kazi hizo na kwamba hakuna ajali iliyowadhuru.

"Tunamwomba mkurugenzi, manyanyaso tuliyokuwa tunapata yaishe. Hatuna mahali pengine ambapo tunaweza kwenda kuuzia matunda yetu zaidi ya hapa maana sisi wateja wetu hawa ni wasafiri wa kwenye magari," alisema Nyabula.

Alisema hata kama wataondolewa basi wapelekwe eneo ambalo magari yatakuwa yanapita ili waendelee kufanya biashara wakiwa na uhakika wa wateja kuwafuata kama ilivyo kwenye eneo hilo.

Naye Rebecca Mwakamela alisema migogoro ya mara kwa mara imekuwa ikiwanyima uhuru wa kufanya shughuli zao na kwamba imekuwa ikiwatengenezea uhasama na viongozi wa serikali akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rungwe.

Alisema kabla ya kumaliza mgogoro huo, walikuwa wana hasira na kiongozi huyo lakini kutokana na busara aliyoitumia kumaliza mgogoro huo mara ya mwisho walimsamehe na hawana kinyongo tena. Wakati wa kusuluhisha mgogoro huo, mkurugenzi huyo aliwataka wajasiliamali kuwa makini wanapoendelea na shughuli zao kwa maelezo kuwa katika eneo hilo wakati mwingine huwa kunakuwa na msongamano wa magari, hivyo kuwa na hatari ya kudhurika na kwamba ndio sababu ya serikali kutaka kuwaondoa.

"Kwa sasa mtaendelea na biashara zenu na sisi tutaendelea kuwatafutia eneo ambalo mtakuwa salama na mtafanya biashara zenu kwa uhuru, lakini pia muendelee kushiriki kwenye shughuli za maendeleo," alisema mkurugenzi huyo.

Kiwira ni miongoni mwa maeneo ambayo maofisa wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) wameweka vibao vinavyozuia wananchi kufanyia biashara lakini bado shughuli hizo zinaendelea.

# Serikali yasitisha kwa muda upondaji kokoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, amesitisha kwa muda shughuli za kuponda kokoto katika viwanda vya matofali hadi serikali itakapotoa mwongozo maalum wa uendeshaji wa shughuli hizo.

Dk. Mkuya alisema hayo jana kwa nyakati tofauti maeneo ya Bumbwini na Mangapwani, Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, alipokuwa katika ziara ya kukagua shughuli hizo na athari wanazozipata wananchi.

Alisema ili kuhakikisha usalama wa mazingira na wananchi, mwongozo umetolewa kuonesha utaratibu wa kufanya shughuli hizo bila ya athari za kimazingira katika siku za baadaye.

Alisema uwapo wa viwanda hivyo karibu na makazi ya watu kunasababisha madhara mbalimbali yakiwamo ya uharibifu wa mazingira, afya na hata vipando vyao.

Aidha, waziri huyo alisema licha ya serikali kuwasisitiza wananchi kuwekeza katika shughuli za kiuchumi, hawapaswi kuchukua kuleta athari ambazo zitavuruga mfumo mzima wa maisha yao.

"Serikali inawataka wananchi wawekeze katika sekta tofauti kwa kuamini kwamba kufanya hivyo ni mwarobaini wa kutatua changamoto hususani za ajira kwa vijana, kuongeza mapato ya mtu mmoja mmoja na serikali kwa ujumla," alisema Dk. Saada.

Alisema zoezi hilo litakuwa endelevu kwa kuangalia viwanda vyote vinavyofanya shughuli hizo ili kuvifanya viwanda hivyo kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kuondoa malalamiko.

Hata hivyo, aliwataka wananchi wanapobaini hitilafu yoyote ya uharibifu wa mazingira kwa namna moja au nyingine ni vyema kuripoti sehemu husika ili serikali ifuatilie na kuchukua hatua za haraka kabla hakujatokea athari. Alisema wapo baadhi ya wawekezaji wanaotoa huduma muhimu kwa jamii ikiwamo kuchimba visima kwa ajili ya kupata majisafi na salama na huduma zingine.

Aliwataka wawekezaji hao kutotumia mwanya huo kwa kuwakandamiza wengine na kila mtu anahaki ya kuishi ndani ya nchi kwa amani bila ya kubughuziwa.

"Kila mwekezaji mwenye uwezo, muhimu kusaidia wananchi kwa namna moja au nyingine katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo, kwani kufanya hivyo mnaisaidia serikali kuweka mazingira mazuri ya maisha ya wananchi," alisema Dk. Saada.

Hata hivyo, aliwataka wawekezaji na wananchi kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayohusiana na uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kulipa umuhimu suala la uhifadhi wa mazingira.

Alisema kufanya hivyo kutaongeza usalama wa afya za wananchi na fursa za ajira na kilimo mambo yatakayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

"Mbali ya uchumi bado tuzingatie usalama wa afya na maisha ya wananchi wetu na hili linawezekana kwa kufanya uwekezaji wa miradi endelevu kwa kuweka kuta zitakazotenganisha maeneo ya uwekezaji na makazi ya wananchi," alisema Dk. Mkuya.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, Sheha Mjaja Juma, alisema ni vyema kwa viwanda vyote vya matofali hivi sasa kufuata utaratibu wa zamani wa kufanya matofali matupu kutokana na rasilimali ya mchanga hivi sasa upatikanaji wake hauna shida.

Mjaja alisema endapo wananchi hao wanataka kufanya biashara ya kusaga kokoto ni vyema mashine zao wakazihamishia maeneo ya kuchimbwa mawe ili kuondoa usumbufu na athari zinazojitokeza katika maeneo hayo.

"Upatikanaji wa mchanga hivi sasa ni rahisi, hakuna usumbufu kama ilivyokuwa siku za nyuma hivyo wamiliki wa viwanda vya matofali mnahitaji matofali kuchanganya na vumbi ili kupata ubora zaidi katika bidhaa hiyo, basi hamisheni mashine zenu mkafanye kazi huko ili hapo kiwandani kuletwe vumbi tu kwa ajili ya kutengeneza bidhaa hiyo," alisema.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi, Idara ya Nishati na Madini, Omar Saleh Mohammed, alisema hivi sasa wapo katika marekebisho kwa baadhi ya kanuni ya maliasili zisizorejesheka na suala hilo likikaa sawa watatoa maelekezo yanayostahiki katika maeneo hayo.

Kwa upande wake, mmoja ya wamiliki wa kiwanda hicho, Soud Abdallah Nassor, alisema malalamiko hayo yapo kwa muda mrefu kutokana na Zanzibar kutotengwa maeneo maalum ya viwanda na makazi ya wananchi.

Alisema hali hiyo husababisha tofauti hizo na kutumia fursa hiyo kuiomba serikali kuliangalia suala hilo kwa upana wake ili kila mtu aishi kwa amani.




Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, kuhusu Siku ya Mtoto wa Afrika. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## 'Watoto wakabiliwa ukiukwaji wa haki zao'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya Zanzibar kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika Juni 16, kila mwaka, bado watoto wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo ukiukwaji wa haki zao za msingi.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku hiyo wizarani kwake, Mnazi Mmoja.

Alisema jumla ya malalamiko 508 ya watoto yamewasilishwa wizarani kwake kwa mwaka 2020/2021 ya ukiukwaji wa haki za watoto.

Alisema malalamiko hayo 251 Unguja na Pemba 257 yamepokelewa, kati ya hayo 347 yanahusiana na watoto kunyimwa matunzo Unguja 139 na Pemba 208 na 161 yanatokana na mvutano wa malezi.

Alisema malalamiko 333 yalipatiwa ufumbuzi na 76 yalitolewa rufaa kwenda mahakamani, wahusika 81 walikubaliana kifamilia na 18 yanaendelea na hatua.

"Katika migogoro hiyo, watoto 1,074 (wanawake 512 na wanaume 562) wa familia hizo waliathirika," alisema.

Aliitaka jamii, familia, mashirika na taasisi mbalimbali ziendelee na uwekaji wa mikakati rafiki itakayowezesha kufanikisha upatikanaji wa haki za watoto na kuimarisha familia kwa kuwadhibiti ili kuwaepusha na ugonjwa wa Covid-19 na vitendo vya ukatili na udhalishaji dhidi yao.

Pia, alizitaka taasisi na jamii kuwa karibu na watoto ili kuwalinda dhidi ya watu wenye nia ovu ndani ya jamii ambapo, hatua hiyo itasaidia kutambua viashiria vyote vya ukatili na udhalilishaji wa aina zote na kujenga jamii bora. "Napenda kusisitiza kuwa suala la malezi bora ni msingi wa mwanzo ambao unaowajenga watoto. Kwa sababu wanahitaji mapenzi, ukaribu na kujengwa uthubutu utakaowawezesha kuwaepusha na matendo yote yanayochangia au kuchochea kuharibu upatikanaji wa haki zao za msingi. Ili kufikia ndoto za maisha yao ya sasa na baadaye," alisema.

Hata hivyo, alisema wizara anayoiongoza inaendelea kutoa misaada ya kiustawi kwa familia zenye watoto wanaoishi katika mazingira magumu na familia 160 (Unguja 91 na Pemba 69) na kinamama 15 (Unguja 11 na Pemba 4) waliojifungua zaidi ya mapacha wawili walipatiwa msaada huo.

# Aagiza kitengo cha damu kuongezewa vitendea kazi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameutaka uongozi wa Wizara ya Afya kuongeza nguvu katika kitengo cha damu salama kwa kuwaongezea vitendea kazi watendaji wao pamoja na kujali stahiki zao ili kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Hemed alisema hayo katika maadhimisho ya siku ya uchangiaji damu duniani, iliyofanyika katika ofisi ya benki ya uchangiaji damu Sebleni, Wilaya ya Mjini Unguja.

Aliwapongeza wafanyakazi wa kitengo hicho kwa kazi kubwa wanayofanya katika kijitoa kwao kuhakikisha wanafikia lengo la ukushanyaji wa damu kwa wingi ili kuokoa maisha ya watu wakiwamo wajawazito, watoto na watu waliopatwa na ajali.

Alisema kutokana na suala la uchangiaji damu kumgusa kila mmoja katika jamii, linahitaji kupewa kipaumbele bila ya kuangalia itikadi za kisiasa, kidini na kikabila.

Makamu wa Pili wa Rais alimuagiza Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuzingatia kuwaweka kwenye nafasi watu wenye uwezo watakaosaidia kuimarisha kitengo hicho cha damu salama.

Alifafanua kuwa, kumekuwapo kwa tabia isioridhisha kwa baadhi ya wakurugenzi katika wizara hiyo kuingilia utendaji kazi wa kitengo jambo ambalo halitoi tija na linawanyima uhuru watendaji waliopo katika kituo hicho.

Akigusia suala la ubunifu, Hemed aliwataka watendaji wanaofanya kazi zao katika kituo hicho kuwa wabunifu kuongeza ufanisi wa kazi badala ya kutegemea bajeti kutoka serikalini. Katika maadhimisho hayo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar aliwapongeza Wakuu wa mikoa na Wakuu wa wilaya kwa ushirikiano wanaouonesha hasa wa kuandaa mabonanza mbalimbali ya uchangiaj damu, akitoa mfano kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa kusaidia kukusanya chupa 1,650 kuwa ni ushirikiano unaotakiwa katika kupeleka mbele gurudumu la maendeleo nchini.

"Nawapongeza sana wakuu wa vikosi vya ulinzi na usalama kwa kuwa mstari wa mbele katika uchangiaji wa damu jambo ambalo linatoa manufaa kwa wananchi," alisema.

Aliwatoa hofu wananchi kuwa wafanyakazi wanaotoa huduma katika kitengo hicho wana utaalamu, weledi na umakini wa kutosha katika kuhakikisha wanalinda afya ya wachangiaji kabla na baada ya kuchangia.

Naye, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazuri, aliwashajihisha watu kuendelea kujitokeza kwa wingi katika uchangiaji damu ili kuokoa maisha ya watu. Alisema, uzoefu unaonesha uhitaji wa damu Zanzibar ni mkubwa zaidi kuliko kiwango kinachochangiwa akitoa mfano kwa mwaka jana uniti 16,000 zilikusanywa, lakini uhitaji wa damu ulifikia kiwango cha uniti 27,000.

# Neema umeme wa uhakika Mtwara, Lindi miradi kimkakati TANESCO

**Na Joseph Mwendapole**



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani. **PICHA: MTANDAO**

SHIRIKA la Umeme (TANESCO), limewekeza kwenye ujenzi wa miradi mikubwa ya kuzalisha umeme lengo likiwa ni kuhakikisha Tanzania inajitosheleza kwa nishati hiyo na kumfikia kila mwananchi kwa gharama nafuu ili waweze kujikwamua kiuchumi kwa kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji.

Ili kufikia azma hiyo TANESCO imekuwa ikitumia vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme kama maji, upepo, jotoardhi na gesi asilia ili kuhakikisha Tanzania inapata umeme wa kutosha na wa bei nafuu ambao kila Mtanzania atamudu kununua.

Wakati akiwasilisha bajeti yake bungeni hivi karibuni, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, aliliambia Bunge kuwa kukamilika kwa miradi mbalimbali ukiwamo wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP), kutawezesha Tanzania kuwa na Megawati 5,000 ifikapo mwaka 2025.

Waziri Kalemani alisema katika kipindi hicho mahitaji ya juu ya umeme Tanzania yanatarajiwa kufikia Megawati 2,677 na kuwa na ziada ya takriban Megawati 2,323 ambayo yatawezesha kuuza kwa nchi jirani zenye upungufu wa nishati hiyo.

Miongoni mwa miradi ya kimkakati kufikia azma hiyo ni wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Mtwara na Somanga Fungo, mkoani Lindi.

### Gesi asilia kuzalisha Megawati 300 Mtwara

Kukamilika kwa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia Mtwara ambao unahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha nishati hiyo kutawezesha kupatikana kwa Megawati 300 na kumaliza matatizo ya umeme kwa Mkoa wa Mtwara.

Kwa mujibu wa Waziri Kalemani, gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 421.1 sawa na takriban Shilingi bilioni 990.47 na kwamba mradi huo unaenda sanjari na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 253 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu.

Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2021/22 kazi zitakazofanyika ni kuanza kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi na kukamilisha taratibu za ufadhili wa mradi huku serikali kupitia TANESCO ikiwa tayari imetenga Sh. milioni 50 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo unaotarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2022 na kukamilika mwezi Agosti, 2024.

### Gesi asilia kuzalisha Megawati 330 Somanga Fungu

Kuhusu mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa Somanga Fungu wa Megawati 330, Waziri Kalemani alisema unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa Megawati 330 kwa kutumia gesi asilia katika eneo la Somanga Fungu, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi.

> **Hadi sasa kazi zilizokamilika ni pamoja na kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa kituo cha kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme na tathmini ya athari kwa mazingira na jamii katika miundombinu wezeshi,**

Waziri alisema gharama za mradi huo zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 423 sawa na Sh. bilioni 994.94 na kwamba mradi huo unaenda sambamba na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 253 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi.

Alisema kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni pamoja na kukamilika kwa upembuzi yakinifu na tathmini ya mazingira na jamii na kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2021/22 ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi na kukamilisha taratibu za ufadhili.

Kwa mujibu wa Waziri Kalemani, utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Februari, 2023 na kukamilika mwezi Desemba, 2025.

### Mradi wa Backbone awamu ya pili

Kuhusu mradi huu, Waziri Kalemani alisema ni wa awamu ya pili ambao unalenga kuongeza uwezo wa vituo vinne vya kupoza umeme vya Iringa, Shinyanga, Singida na Dodoma kutoka kV 220 mpaka kV 400.

Alisema awamu ya kwanza ya mradi ulihusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga kupitia Dodoma na Singida wenye urefu wa kilomita 670.

Aidha, Waziri alisema mradi huo ulikamilika mwezi Desemba 2016 kwa asilimia 100 na kwa sasa unaendeshwa kwa msongo wa kV 220 na kwamba awamu ya pili gharama ni Dola za Marekani milioni 120 sawa na Sh. bilioni 282.25.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa vituo vya Singida na Dodoma utekelezaji wake kwa ujumla umefikia asilimia 95, kukamilisha ununuzi wa vifaa na kupata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Iringa na Shinyanga.

Waziri alisema katika mwaka wa fedha wa 2021/22 kazi zitakazofanyika ni kukamilisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Dodoma na Singida na kuendelea na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Iringa na Shinyanga.

Kwa mujibu wa Waziri Kalemani, jumla ya Sh. bilioni 12.59 fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo na utekelezaji wa mradi huo ulianza mwezi Julai, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2022.

Kuhusu mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi, waziri alisema mradi huo utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 198 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi, mkoani Dar es Salaam.

Waziri alisema gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 150 sawa na takriban Sh. bilioni 352.82 na kuwa zilizofanyika hadi sasa ni pamoja na kudurusu taarifa ya upembuzi yakinifu ili kujumuisha njia ya kusafirisha umeme kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha JNHPP kupitia Kibiti na kuendelea na malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2021/22 kazi zitakazofanyika ni kuendelea na taratibu za kupata ufadhili wa mradi na kukamilisha malipo ya fidia.

Dk. Kalemani alisema jumla ya Sh. bilioni 8.53 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo na utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwezi Desemba 2021 na kukamilika mwezi Mei 2023.

### Uwekezaji katika miradi midogo ya Nishati Jadidifu

Kuhusu miradi hii, Waziri Kalemani alisema serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia na kudhibiti uendelezaji wa miradi midogo ya nishati jadidifu nchini kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu, kuongeza mchango wa nishati hiyo katika uzalishaji umeme na kutunza mazingira.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2020/21, serikali kupitia EWURA ilidurusu kanuni za kusimamia uendelezaji wa miradi midogo ya umeme chini ya MW 10 "The Electricity (Development of Small Power Projects) Rules, 2020" na kutangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 3 Julai, 2020.

Alisema kukamilika kwa kanuni hizo kumeiwezesha TANESCO kuingia makubaliano na Kampuni saba za Wawekezaji binafsi wa Miradi Midogo ya Umeme kwa kusaini mikataba ya kuuziana umeme (Standardized Small Power Projects Agreements - SPPA).

Alizitaja kampuni zilizosaini SPPA na TANESCO kuwa ni NextGen Solawazi Ltd (Umeme Jua MW 5 - Kigoma), SSI Energy Tanzania Ltd (Umeme Jua MW 10 - Kahama), Lung'ali Natural Resources Company Ltd (Maji MW1.28 - Kilolo), Luponde Hydro Ltd (Maji MW 1 - Njombe), Nishati Lutheran (DKK), Investment Ltd (Maji kW 360 - Makete), Madope Hydro Company Ltd (Maji MW 1.7 - Ludewa) na Turiani Hydropower Company Ltd (Maji MW 5 - Mvomero).

Alisema EWURA imetoa leseni moja (1) ya kuzalisha umeme wa MW 2.4 kwa kutumia nishati jadidifu ya upepo kwa kampuni ya Mwenga Hydro Ltd na mradi huo wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo ni wa kwanza nchini na umeme unaozalishwa unasambazwa katika maeneo yanayohudumiwa na kampuni hiyo katika Wilaya ya Mufindi na umeanza uzalishaji umeme mwezi Novemba, 2020.




# KOCHA HISPANIA AMTETEA MORATA

**SEVILLE,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Hispania, Luis Enrique na wachezaji wake, wamemtetea Alvaro Morata baada ya kuzomewa katika mchezo wa suluhu dhidi ya Sweden kwenye michuano ya Euro 2020.

Morata alipata nafasi nzuri sana ya kufunga bao kwenye mchezo huo wa kwanza wa Hispania kwenye michuano hiyo katika Kundi E, lakini akampasia golikipa wa Sweden, Robin Olsen, juzi Jumatatu.

Hispania ilitawala mchezo wote uliopigwa hapa Seville wakati ikipiga pasi 917 na kutawala mchezo kwa asilimia 85, lakini walishindwa kabisa kupata bao.

Morata alizomewa na mashabiki wa Hispania kwa kupoteza nafasi hiyo ya kufunga na alitolewa dakika ya 66.

"Alifanya kazi yake uwanjani na ningependa zaidi kumsifia," alisema Luis Enrique baada ya mchezo huo akiwaambia waandishi wa habari.

"Morata ni mchezaji mkubwa ambaye anafanya makubwa na mazuri kwenye safu ya ushambuliaji.

"Nilisikia kuzomewa kwa Morata, lakini alitakiwa kupongezwa. Alifanya mambo mengi kwa timu, lakini sidhani kama hilo litamuathiri"

# Ronaldo: Naifikiria Ureno kwanza si Juventus

**LISBON,** Ureno

CIRISTIANO Ronaldo alionekana mbele ya waandishi wa habari kuzungumzia mambo yote ya Ureno kabla ya kampeni yao ya Euro 2020 kuanza jana Jumanne, lakini alibanwa wakati mmoja juu ya hatima yake katika klabu yake ya Juventus.

Kumekuwa na ripoti nyingi zinazomhusisha Ronaldo kuondoka Juventus msimu huu wa majira ya joto, lakini aliweka wazi kuwa uvumi huu hauhitaji kushughulikiwa sasa hivi.

"Nimekuwa nikicheza kwa kiwango cha juu kwa miaka 18, hiyo hainisumbui hata kidogo," alisema Ronaldo wakati wa mkutano na waandishi wa habari alipoulizwa juu ya uvumi kama unamwathiri.

"Chochote kitakachotokea, kitakuwa ni bora. Bila kujali kama nitakaa (Juventus) au nitaondoka, hilo si jambo la muhimu zaidi kwa sasa.

"Ninazingatia timu yangu ya taifa, kwa sababu haichezi mashindano ya ukubwa huu kila siku. Ni mashindano yangu ya tano ya Ulaya, lakini kwa akili yangu ni kana kwamba ni ya kwanza."

Ureno ilishinda Euro 2016 baada ya kuifunga Ufaransa kwenye fainali na mwaka huu ni moja ya timu inayopewa nafasi kushinda michuano hiyo.





# Mbappe azinguana na Giroud

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amekiri kwamba, "aliathiriwa" na malalamiko ya Olivier Giroud juu ya wachezaji wenzake wa Ufaransa kutompatia pasi, lakini amesisitiza kuwa hakutaka kulifanya jambo hilo kuwa kubwa.

Giroud alisema baada ya timu yake kukipiga na Bulgaria katika mchezo wao wa mwisho wa kirafiki kwamba, alikuwa hapokei pasi licha ya kukimbia kwenye maeneo hatari katika boksi.

Maoni hayo yalipokelewa tofauti na Mbappe na nyota huyo wa Paris Saint-Germain, amesema angependelea kama Giroud angezungumza naye kwa faragha badala ya kutoa malalamiko yake kwa waandishi wa habari.

"Nilizungumza na Olivier Giroud. Kila mtu anajua kilichotokea," Mbappe alisema katika mkutano na waandishi wa habari.

"Ni kweli kwamba niliathiriwa naye kidogo. Lakini hatutafanya jambo hili kuwa kubwa kwa sababu tuko hapa kuiwakilisha Ufaransa, hilo ndilo jambo muhimu zaidi.

"Alichosema hakikunisumbua zaidi ya hapo, mimi ni mshambuliaji na nimekuwa na hisia hii mara 365 kwenye mchezo."

'Les Bleus' jana Jumanne walianza kampeni yao ya Euro 2020 kwa mchezo wa kwanza dhidi ya Ujerumani.

# MARCELO KUBAKI REAL MADRID



**MADRID,** Hispania

MARCELO ataendelea kukaa Real Madrid kwa msimu wa 2021/22 ukiwa ndio mwaka wake wa mwisho kwenye mkataba wake unaomalizika Juni 2022.

Beki huyo wa kushoto alitajwa kama mmoja wa wachezaji ambao wangeweza kuhama msimu huu wa joto, lakini aliwasiliana na wakurugenzi wa klabu kuzungumzia hali yake.

Mbrazil huyo ana uhusiano mzuri na viongozi wa hapo Santiago Bernabeu na walimhakikishia kwamba hakukuwa na chochote cha kuwa na wasiwasi juu yake.

Maoni ya kocha mpya, Carlo Ancelotti pia yamekuwa sababu katika uamuzi wa kumbakisha Marcelo, huku Muitaliano huyo akiwa amemtumia beki huyo mara 53 katika msimu wa 2014/15. Hiyo ndiyo idadi kubwa zaidi ya mechi ambazo Marcelo amefanikiwa kwa mwaka mmoja kama mchezaji wa Real Madrid.

Marcelo hakuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara nafasi ya mlinzi wa kushoto kwani jukumu hilo alipewa Ferland Mendy na Miguel Gutierrez alipewa muda wa kucheza nafasi hiyo kuelekea mwisho wa msimu uliopita na bado ana matumaini mazuri.

Real Madrid bado inamshikilia sana Marcelo, ingawa umri wake unaonekana kuwa mkubwa na anaweza hata kuwa nahodha mkuu ikiwa Sergio Ramos ataondoka.

## Liver yamwongezea mkataba Adrian



**LIVERPOOL,** England

GOLIKIPA wa Liverpool, Adrian, amesaini mkataba mpya wa kuendelea kukaa hapo kwenye dimba la Anfield kwa msimu ujao.

Msaidizi huyo wa Alisson, Adrian raia wa Hispania alijiunga na klabu hiyo akiwa mchezaji huru mwaka 2019, akicheza mechi 24 kwa 'Wekundu' hao.

Kipa huyo wa zamani wa West Ham, ameshinda taji la Ligi Kuu England, UEFA Super na Klabu Bingwa Dunia katika muda wake hapo Anfield.

Alicheza mechi sita katika mashindano yote msimu huu ulioisha, huku akicheza mechi tatu bila kuruhusu nyavu zake kutikiswa.

"Nimefurahishwa na nina furaha kuendelea kuwa kwenye klabu hii," alisema Adrian akiiambia tovuti ya Liverpool. "Kwanza kwa sababu ni kama zawadi kutoka kwa klabu baada ya kufanya kazi kubwa ambayo nimeifanya tangu niliposajiliwa hapa miaka miwili iliyopita.

"Kwa hakika kabisa nashukuru kwa klabu kuniamini, kocha pamoja na kila mmoja hapa.

"Pili nina shauku kubwa ya kuendelea kucheza hapa kwa misimu mingine mingi zaidi."

## *Sancho afunguka shabiki Chelsea*

**LONDON,** England

JADON Sancho amekiri kwamba, utotoni alikuwa shabiki mkubwa wa Chelsea wakati akifunguka juu ya uvumi unaomhusisha na kuhamia Manchester United.

'Mashetani Wekundu' hao walijaribu na kushindwa kumshawishi Sancho aondoke Borussia Dortmund mwaka jana wakati kocha Ole Gunnar Solskjaer alitaka kuimarisha kikosi chake.

United kwa mara nyingine wamemtambua kijana huyo wa umri wa miaka 21 kama lengo lao kubwa kabla ya dirisha la uhamisho wa majira ya joto, na tayari wametoa ofa ya pauni milioni 67 ambazo zilikataliwa.

Lakini sasa Sancho amekiri kwamba, yeye alikuwa mnazi mkubwa wa Chelsea wakati wa utoto wake, ingawa hajaweka wazi kama bado ana mapenzi nayo kwa sasa.

Alipoulizwa kutaja mfano wake kuigwa wa mpira wa miguu wakati wa ujana wake, Sancho aliiambia talkSPORT: "Labda ningesema Frank Lampard. Nilikuwa shabiki wa Chelsea nikikua, siwezi kusema uwongo.

"Didier Drogba na Frank Lampard walikuwa wachezaji ninaowapenda wakati huo.

"Nampenda sana Frank Lampard na jinsi alivyocheza mchezo wake; ulikuwa wa moja kwa moja na hivyo alifunga sana.

"Na mimi ninapenda vitu kama hivyo."

Kuhusu kutakiwa Man United, Sancho alisema kwa sasa hawezi kulizungumzia hilo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI ALIA NA UWANJA KUWANYIMA USHINDI

●●● Ni baada ya kufunga wakilazimishwa sare na Chile kwenye Copa America juzi...

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

LIONEL Messi amesema Argentina ilishindwa kutawala mchezo na amelaumu hali ya uwanja wakati wakitoka sare na Chile kwenye mchezo wao wa kwanza wa michuano ya Copa America, juzi.

**Messi alifunga bao la uongozi kwa mkwaju wa adhabu ndogo kipindi cha kwanza, lakini halikutosha kuweza kupata ushindi dhidi ya Chile ambao walisawazisha na matokeo kusomeka 1-1, kwenye mchezo huo wa Kundi A uliopigwa hapa Rio de Janeiro, Jumatatu.**

Nyota na nahodha huyo, Messi aliifungia Argentina bao hilo la adhabu ndogo kwa mara ya kwanza tangu Novemba 2016 - baada ya siku 1,672 - lilitokana na Claudio Bravo kufanyiwa faulo dakika ya 33.

Nyota wa Chile, Arturo Vidal alizawadiwa penalti kutokana na kukwatuliwa na Nicolas Tagliafico baada ya mwamuzi, Wilmar Roldan kuangalia marudio kwenye Tv, lakini alishindwa kuikwamisha nyavuni baada ya kuokolewa na golikipa Emiliano Martinez.

Dakika moja baadaye Eduardo Vargas akafunga bao la kusawazisha lile la Messi katika kipindi cha pili.

"Nafikiri penalti na bao la kusawazisha kuliwapa amani ya moyo, kwani walijaribu kumiliki mpira, sisi hatukuweza kutawala mchezo kabisa," alisema Messi, ambaye bao hilo la adhabu ndogo lilikuwa la tatu kwenye michuano ya Copa Amerika, akiwaambia waandishi wa habari.

"Wakati tulipopata nafasi hatukuweza kuwa kwenye ubora wetu na tukashindwa kupata matokeo tuliyoyataka.

"Dimba la kuchezea halikutusaidia, uwanja haukuwa kwenye hali nzuri na tukashindwa kumiliki mpira mara kwa mara. Hata penalti waliyopewa sidhani kama ilistahili na ndio iliyobadilisha kabisa mchezo."

Argentina ambao ni washindi wa pili wa michuano hiyo mwaka 2015 na 2016 wanaonolewa na kocha, Lionel Scaloni, hawakuonekana tishio sana mbele ya vijana hao wa Chile.

"Tulitaka kuanza kwa ushindi, ilikuwa ni muhimu kupata ushindi," aliongeza kusema Messi.

"Tulicheza dhidi ya timu ngumu na sasa tutacheza na Uruguay, timu nyingine ngumu sana kwetu."

## ZISIKUPITE

### RONALDO ANAONDOKA

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, kwa mara nyingine tena hajakataa uwezekano wa yeye kutimka Juventus, kabla ya kumalizika kwa mkataba wake mwakani. Anahusishwa na klabu yake ya zamani ya Manchester United, huku Klabu hiyo ya Italia, ikitarajiwa kutengeneza fedha ndefu kupitia straika huyo. ***(Express)***

### TIERNEY ATAKIWA CITY

MLINZI wa kushoto wa Arsenal na Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 24, amehusishwa na uhamisho wa kuhamia Manchester City. Kocha wa zamani wa Celtic, Neil Lennon, ndiye anayemhusisha nyota huyo na uhamisho huo. ***(Times)***

### VARANE AWANIWA PSG

MLINZI wa kati wa Real Madrid, Raphael Varane anatarajia kutimka kwa wababe hao wa Hispania, huku klabu za Manchester United na Paris Saint Germain (PSG) zikionyesha nia ya kumtaka. Inaonekana nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, angependelea kutua PSG ambao watalazimika kulipa kitita cha pauni milioni 51.5. ***(El Confidencial, via Caught Offside)***

### SANCHO HUYOOO UNITED

WINGA wa England, Jadon Sancho anatarajia kujiunga na Manchester United, licha ya Borussia Dortmund kukataa dau la awali la pauni milioni 67 kwa ajili ya kinda huyo mwenye umri wa miaka 21. Klabu hiyo ya Bundesliga inang'ang'ania dau la pauni milioni 77. ***(Manchester Evening News)***

### GREALISH KUTUA CHELSEA

CHELSEA wanapewa nafasi kubwa ya kumnasa kiungo wa England na Aston Villa, Jack Grealish msimu huu, wakitarajiwa kuzipiku klabu za Jiji la Manchester, kwenye mbio za kupata saini ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Fichajes via Mirror)***

### DILI LA XHAKA ROMA GUMU

UHAMISHO wa kiungo wa Uswisi, Granit Xhaka kutoka Arsenal kwenda AS Roma inayonolewa na Jose Mourinho, hautarajiwi kukamilika mapema kwa sababu klabu hizo zimekutana na kuna mkwamo katika mazungumzo ya uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 28. ***(Corriere dello Sport via Express)***

### PHILLIPS AWINDWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United imemwongeza mlinzi wa Liverpool, Nat Phillips katika orodha ya wachezaji inaowafukuzia, lakini itawalazimu kupambana na Burnley kumnasa beki huyo wa kushoto raia wa Uingereza, ambaye hatarajii kupata nafasi watakapopona majeraha Virgil Van Djik, Joe Gomez na Joel Matip. ***(Mail)***

### SOUMARE SAFI LEICESTER

LEICESTER City inatarajiwa kukamilisha usajili wa kiungo Mfaransa, Boubakary Soumare wiki hii. Klabu za Wolves na Everton nazo zinavutiwa na kinda huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye kwa sasa anachezea mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa (Ligue 1) Lille. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# SIMBA, YANGA ZATANGULIA NUSU FAINALI YA VIJANA U-20

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Simba na Yanga, chini ya miaka 20, zimetinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Vijana chini ya miaka 20, baada ya kushinda mechi zao ilizocheza juzi usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Yanga ndiyo ilianza kutinga hatua hiyo saa 1:00 usiku ilipoiadhibu bila huruma, Mwadui FC mabao 3-0 na kumaliza Kundi A ikiwa na pointi saba na mabao matano.

Vijana wa Yanga, wakiongozwa na winga wa zamani wa timu hiyo, Said Maulid 'SMG', walipata mabao yao kupitia kwa Abdulkarim Yunus aliyefunga mawili na Abby Mikimba aliyefunga bao moja.

**Mechi zao zilizopita, Yanga ilitoka suluhu, bila kufungana na watani zao wa jadi, Simba na baadaye kuichapa JKT Tanzania mabao 2-0.**

Timu ya Vijana ya Simba nayo ilisonga mbele baada ya kuifunga JKT Tanzania bao 1-0, mechi ikichezwa kwenye uwanja huo huo, saa 3:00 usiku.

Kwa ushindi huo Simba inamaliza mechi zake za Kundi A ikishika nafasi ya pili nyuma ya Yanga, kwani baada ya kutoka suluhu na vinara hao, walishinda bao 1-0 dhidi ya Mwadui, hivyo kuzidiwa kwa idadi ya mabao ya kufunga.

Timu hizo sasa zitasubiri timu mbili kutoka Kundi B kujua wapinzani wao wa kucheza hatua ya nusu fainali. Kundi hilo lina timu za Azam na Mtibwa Sugar ambazo zina pointi nne, Prisons ikiwa na pointi tatu, huku Kagera Sugar ikiwa haina pointi yoyote.

HESABU...



Mshambuliaji wa Taifa Stars, Yusuph Mhilu, akipiga hesabu ya kumtoa beki wa Malawi kwenye mechi ya kimataifa ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili na Stars kushinda 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Marathon zarejeshwa Z'bar kutangaza utalii*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAIMU Waziri wa Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo, Lela Mohammed Mussa, amesema mpango wa kufufua mashindano ya mbio za Marathon Zanzibar, unalenga kutangaza vivutio vilivyomo ili kuongeza idadi ya wageni nchini.

Kesho kutwa Ijumaa kutakuwa na mbio za kilomita tano, 10 na 21 ambapo mbali na washiriki kutoka Zanzibar na Tanzania Bara, zitajumuisha wakimbiaji kutoka nchi mbalimbali, huku zikipitia Mji Mkongwe na kuishia katika Uwanja wa Amani.

Akizindua mbio hizo za Zanzibar International Marathon katika Hoteli ya Park Hyatt mjini hapa, Waziri Lela alisema ili kuona dhana ya utalii kwa wote inafanikiwa ni vema kuinua mambo yatakayoifanya Zanzibar kutamkwa zaidi duniani.

Alisema mashindano kama hayo yaliwahi kufanyika Zanzibar na kuifanya kutambulika kimataifa, hivyo kuanzishwa tena kwa sasa kunahitaji mikakati imara ili kuwa endelevu.

Waziri Lela ambaye ni Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, alisema serikali iliyopo madarakani chini ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, ipo tayari kufanya kazi na sekta yoyote ikiwamo ya michezo kwa nia ya kuinua uchumi wa nchi hasa ukizingatia kuwa lengo lake ni kupata medali 100 za dhahabu kupitia michezo mbalimbali.

Aidha, alisema serikali inakusudia kuimarisha michezo mbalimbali ikiwamo marathon na kuwapongeza waandaaji wa mashindano hayo kwa kuwa walionyesha mwanzo mzuri wa kutaka kuibua vipaji na kutoa ajira kupitia tasnia hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya mashindano hayo, Hassan Suleiman Zanga, alisema mashindano hayo yana lenga kuunga mkono juhudi za serikali katika kuitangaza Zanzibar ambayo imewahakikishia wageni kuendelea kuwa salama chini ya uongozi wa Dk. Mwinyi katika fursa zinazotokana na uchumi wa buluu.

Aidha, alisema asilimia 20 ya fedha zitakazopatikana katika mbio hizo zitakwenda kwa wazee wa Zanzibar.

## Majembe ya CAF Simba Queens J'2

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umesema Jumapili wiki hii utaweka wazi mikakati yao ikiwa ni pamoja na kutangaza majembe mapya kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika kwa upande wa timu ya wanawake, Simba Queens.

Simba Queens ambao mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, itaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao kwa mara ya kwanza.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema baada ya kumaliza ligi msimu huu, walikutana na uongozi wa timu hiyo na kuweka wazi mapendekezo yao na tayari yameshaanza kufanyiwa kazi.

Alisema tayari suala la usajili limefanyiwa kazi na Jumapili hii wataweka wazi nafasi na majina ya wachezaji ambao wamewasajili kwa ajili ya michuano hiyo ya kimataifa.

"Katika usajili wetu tumeangalia zaidi michuano ya kimataifa, kulingana na mahitaji hayo usajili wetu tumetupia jicho zaidi nje ya Tanzania ili kukiimarisha kikosi chetu kuelekea michuano hiyo," alisema Mgosi.

## Miss East Africa 2021 kufanyika D' Salaam

**Na Sabato Kasika**

MASHINDANO ya kumsaka Miss East Africa 2021, yanatarajia kufanyika jijini Dar es Salaam Novemba mwaka huu na kushirikisha nchi 15.

Makamu Rais wa Mashindano hayo, Jolly Mutesi, alisema ni fursa nzuri kwa Tanzania kujitangaza kupitia utalii na uwekezaji na kwamba kwa mwaka huu yameandaliwa na Rena Events Limited ya Dar es Salaam.

Mutesi ambaye yupo nchini kwa ziara ya wiki mbili kwa ajili ya maandalizi ya awali, alisema, mashindano hayo ni makubwa ya urembo kwa ukanda huu wa Afrika Mashariki yakitarajiwa kuangaliwa na watu wengi duniani.

Mutesi alizitaja nchi zitakazoshiriki mbali na mwenyeji Tanzania kuwa ni Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Ethiopia, Eritrea, Djibouti, Somalia, Madagascar, Malawi, Ushelisheli, Sudan Kusini, Comoro na Mauritius.

Mashindano hayo ambayo yalibuniwa na kuanzishwa na Rena Callist, yalianza mwaka 1996 na kuwahi kufanyika Burundi kwa udhamini wa Hayati Rais Piere Nkurunzinza.

# Michezo

Jumatano Juni 16, 2021

Nipashe



Mbappe azinguana na Giroud Ufaransa UKURASA 20

**WATUPIAJI...**



Wafungaji wa mabao wakati timu zao zikitoka sare ya bao 1-1 kwenye mchezo wa fainali za Copa America uliyopigwa Uwanja wa Nilton Santos jijini Rio de Janeiro, Brazil juzi, Lionel Messi wa Argentina na Eduardo Vargas wa Chile (kulia) wakipambana katika mechi hiyo ya Kundi A. **PICHA: MTANDAO**

## Watano wapeta kuwania urais ZFF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imepitisha majina matano ya wagombea urais wa shirikisho hilo katika uchaguzi mdogo unaotarajiwa kufanyika mapema mwezi huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa kamati hiyo, Makungu Omar Makungu, alisema wagombea watano waliochukua fomu ya kuwania nafasi hiyo na kuzirejesha wamekidhi vigezo vilivyopo kwa mujibu wa Katiba ya ZFF huku wawili wakishindwa kuzirejesha.

Wagombea waliorejesha fomu na kupitishwa katika kinyang'anyiro cha urais ni Abdulatif Ali, Suleiman Shaban Suleiman, Suleiman Mahmoud Jabir, Haji Shehe Hamad na Abdulkadir Mohmed Abdulkadir "Tash".

Makungu aliwataja wagombea wawili ambao hawakurejesha fomu kuwa ni Mbarouk Othaman pamoja na Mudrik Majaaliwa Mwinyi. Alisema kwa mujibu wa ratiba ya Kamati ya Uchaguzi ya ZFF, kuanzia jana Juni 15 hadi Juni 18, mwaka huu ni muda wa pingamizi kwa wagombea.

Uchaguzi huo wa ZFF unafanyika kutokana na kujiuzulu kwa aliyekuwa Rais wa shirikisho hilo, Seif Kombo Pandu mapema Februari mwaka huu.

# RAIS SAMIA ATAKA NYASI BANDIA VIWANJA CCM

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Ni baada ya kusamehe kodi, akitaka chama hicho kikishindwa sasa kukaribisha wawekezaji ili...

KILIO cha ubovu wa viwanja vya soka nchini, sasa kinakaribia kupata suluhisho la kudumu baada ya Rais wa Jamburi ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kukitaka Chama Cha Mapinduzi (CCM), kuboresha viwanja vyao vya soka ili visaidie kuinua michezo nchini.

**Mkuu huyo wa nchi, alitoa agizo hilo jana alipozungumza na vijana jijini Mwanza, ambapo alisema serikali imeondoa kodi katika uingizaji wa nyasi bandia, hivyo akaagiza CCM kutumia fursa hiyo kuboresha viwanja vyao na kama chama hicho hakina uwezo wa kutekeleza kazi hiyo chenyewe, kiingie ubia na wawekezaji.**

Idadi kubwa ya viwanja vya soka vinavyotumika katika michezo ya Ligi Kuu Bara na ligi za madaraja mengine nchini, vinamilikiwa na CCM, na kwa muda mrefu chama hicho kimekuwa kikilalamikiwa kwa kushindwa kuviboresha hususan eneo la kuchezea 'pitch'.

Baadhi ya viwanja vya soka vinavyomilikiwa na chama hicho na mikoa viliko kwenye mabano ni Kambarage (Shinyanga), Kirumba (Mwanza), Ali Hassan Mwinyi (Tabora), Karume (Mara), Mkwakwani (Tanga) na Sheikh Amri Abeid (Arusha).

Hoja ya kutaka kukarabatiwa kwa viwanja hivyo ilianzia kwa Mbunge wa Makete, Festo Sanga, ambapo wiki chache bungeni wakati akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, alimwomba rais kuingilia kati suala la viwanja vya mpira wa miguu nchini vinavyomilikiwa na CCM ambavyo vimegubikwa na "mchakato" katika kuviboresha.

Sanga alimwomba rais asaidie viwanja hivi viwekwe nyasi bandia ili visaidie kukua kwa michezo nchini kwa kuondoa kodi kwa maslahi ya soka hapa nchini.

Hata hivyo, wakati akiwasilisha Makadirio ya Bajeti ya Serikali, kwa mwaka 2021/22 bungeni jijini Dodoma Juni 10, mwaka huu kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa, serikali ilipendekeza kusamehe ongezeko la thamani kwenye nyasi bandia kwa viwanja vya mpira wa miguu kwenye majiji kwa ajili ya kuendeleza michezo na kukuza vipaji nchini.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha makadirio hayo alisema kwa mwaka huu wa fedha, anapendekeza kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye nyasi bandia kwa ajili ya viwanja vya mpira wa miguu vya majiji, huku kukiwa na lengo la kufanya hivyo kwenye manispaa, viwanja hadi kwenye timu wakati wa bejeti zijazo.

"Mheshimiwa Spika, viwanja vyetu vingi ni vibovu sana, labda ukiacha kile cha Majaliwa Lindi. Vingi ni vibovu. Na ubovu wa viwanja hivyo unasababisha timu bora kama Yanga inashindwa kupata matokeo mazuri inapokwenda mikoani," alisema waziri huyo na kusababisha vicheko na makofi kutoka kwa baadhi ya wabunge.

Kauli hiyo ya Rais Samia, imekuja wakati muafaka ambao soka la Tanzania linazidi kupiga hatua na endapo viwanja hivyo vitaboreshwa Ligi Kuu Bara itazidi kuwa kivutio kwa wawekezaji wengi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >